Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

... Na kama Mwenyezi Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi...
(Al-Hajj 22:41)

JUZU 74 No. 171 | MUHARRAM 1434 AH | DECEMBER 2012 | FATAH 1391 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa wa Islam atoa hotuba ya kihistoria katika bunge la Umoja wa Ulaya na kusisitiza: Islam katu haihamasishi vurugu

Na Mussa Awadhi Mpinga - Dar es Salaam



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a, Khalifatul Masih V, akihutubia wajumbe wa Umoja wa Ulaya Brussels, Ubelgiji.

Habari kamili uk 3

Msikiti wa Kwanza wa Ahmadiyya mjini Lindi wafunguliwa

Na Sheikh Waseem A. Khan - Dar es Salaam



Kwa msaada wa Allah Karim Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya Tanzania imeweza kukamilisha Msikiti mzuri mwingine katika mji wa Lindi ambao ufunguzi wake rasmi ulifanywa tarehe 23 Oktoba 2012.

Endelea uk. 4

Adabu katika kukutana na Khalifa wa zama

Imeandikwa na Hadhrat Khalifatul Masih II (ra)

Katika hafla ya Jalsa Salana, kukutana na Khalifa ni jambo la muhimu sana. Hata hivyo, kuna nukta chache zinazofaa kuzingatiwa.

Kwanza kabisa, Khalifa hapokei Baiat kwa utashi wake tu, bali Baiat huchukuliwa kwa kumwakilisha Mtume. Katika mwendeleo wetu, mwanzilishi wa Ahmadiyyat alifikia uwakilishi wa Mtume Mtukufu (saw) na Khalifa hufikia uwakilishi wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Ifahamike kuchukua Baiat kwa mkono wa Mtume Mtukufu (saw) kunatambulika kama kuchukua Baiat kwa mkono wa Mungu Mwenye Enzi. Hivyo, kwa vile mkono wa Khalifa umefikia uwakilishi wa Mtume, kwa hivyo, kupeana mkono na Imamu wa zama kuna baraka vile vile.

Lakini sio aina ya kupeana mikono kama inayotokea katika kundi au genge la watu ambamo maumivu kiasi yatasikika na wewe na maumivu mengine nitayahisi mimi. Kupeana mikono huku ni kule kunakofanywa wakati wa mkutano. Ingawa, katika wakati ule kuna muda mchache tu kwa ajili ya kupeana mikono, inapaswa ikumbukwe kwamba Mungu,

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Lazima au 'Inshallah'

Matumizi ya neno lazima yana chembe chembe za majivuno, kunata na kujisahau. Hizi katu si sifa za mja ambaye kwa kipimo chochote utakachotumia yeye "binadamu ni dhaifu tena ni dhaifu sana", kama alivyoimba Ustadh Hamisi Sultani Wamwera.

Mwaka 1917 Muasisi wa taifa la Urusi Viadmir Ilynach Lenin alitumia sana tena kwa mbwembwe neno 'Lazima'. Sera ya ujamaa lazima ishinde, lazima ienee kila pembe ya dunia, lazima wafanyakazi na wakulima washinde. Naam Urusi ilitamba, ikatikisa dunia, ikawa na majeshi makubwa chini ya muungano wa Warsaw ambao ulikuwa ni umoja wa kujihami wa nchi za kijamaa. Neno hili 'Lazima' likarithiwa na viongozi waliofuata akina Stalin. Matokeo yake Urusi ilipiga mweleka wa kisiasa tarehe 25 Disemba 1991 na Urusi imebaki kuwa na mvuto kwa wanafunzi tu wa Historia. Neno 'Lazima' limezikwa pamoja nao kwa hao waliojigamba na kujitutumua.

George W. Bush aliambiwa hizo silaha za maangamizi huko Iraq ni hadaa na nia yake ni kutafuta mafuta. Kama aliyetoka usingizini alitangaza lazima tuivamie Iraq, lazima tumuondoe Sadamu Hussein. Lazima hiyo imesaidia nini Iraq? Watu wangapi wamekufa kwa sababu ya neno hilo 'Lazima'. Waamerika wangapi wamerudi katika masanduku kutoka Iraq? Je Bushi hakujifunza kutoka kwa mshairi wa Marekani Walt Whiteman kuwa; "Je tulidhani ushindi ni kitu kikubwa"?
Utamaduni huu kwa bahati mbaya umebisha hodi barani Afrika. Utamsikia kiongozi bila kujali masika au kiangazi akitamba 'Lazima' chama chake kishinde. Lazima sera waliyoitunga ishinde. Huku ni kughafirika, huku ni kusahau, na binadamu mwenzio anapokosea ni wajibu kumkumbusha. Yupo Kiongozi aliyetangaza Kadamnasi kwamba angeweza kumuona Rais ajaye, bahati hiyo hakuipata.

Ghamal AbdulNasar mwaka 1967 alitangaza 'Lazima' tutashinda na tutaiangamiza Israel. Muulize Mohamedi Heikal neno hilo 'Lazima' liliishia wapi? Kwame Nkurumah naye wa Ghana alighafirika. Aliahidi 'Lazima' nitarudi Accra. Muulize Profeda Alli Mazrui nini kilichotokea.

Kuna aina fulani ya ulevi, kiongozi anapokuwa jukwaani akihutubia. Anapenda kufurahisha na kuvuta hisia za wasikilizaji. Hilo si jambo baya, baya ni kujisahau wewe ni nani? Leo upo kesho haupo. Leo unashinda kesho unashindwa. Na huo ndio mtiririko wa maisha ya mwanadamu. Kukiri unyonge wetu na udhaifu wetu ni sifa zinazosaidia katika ujenzi wa Taifa. Hakuna lolote linaloweza kufanyika bila Mwenyezi Mungu kupenda. Tunapopanga lolote na kuahidi kufanya lolote tukumbuke kutanguliza neno "MUNGU AKIPENDA". Neno hili linaweza kuwa dawa mjarabati kwa matatizo yanayolikabili bara letu la Afrika.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Adabu katika kukutana na Khalifa wa zama

Kutoka uk. 1

Mwenye Enzi hutimiza baraka za wateule wake na Makhalifa katika kitambo kidogo tu cha wakati. Kama wasingekuwa na sifa hii, hapo wasingeweza asilani kutekeleza kazi yao. Hivyo wakati wa kupeana mikono, maombi hufanywa kimahsusi. Pamoja na hayo, adabu inapaswa kutiliwa maanani.

Haipaswi kutokea kwamba mtu aliyembali katika mstari ananyoosha mkono wake, na mwingine anauvuta kwa nyuma. Ikiwa muda wa kupeana mikono umekwisha basi uachwe upite, lakini kupeana mikono kufanywe kwa utaratibu kutokea mstari wa mbele. Hii ndio sababu nimetenga muda wa kukutana na mtu mmoja mmoja, ili kila mmoja apate nafasi ya kupeana nami mkono.

Halafu baadhi ya watu wana maoni kwamba ni lazima kutoa zawadi ya fedha wakati wa kupeana mikono au kukutana (na Khalifa). Hivyo wengine wanaacha kuonana na Khalifa kwa kuwa hawana fedha za kutoa. Lakini wazo hili ni baya. Jambo hili (la kutoa zawadi ya fedha) kwa kweli halina uhusiano wowote na kupeana mikono au kukutana na Khalifa.

Mungu Mwenye Enzi Anasema; 'WAKUUNUU MA'AS-SAADIKINA' (Na kaeni pamoja na wakweli) Qurani Tukufu 9:19. Mtu anayepeana mkono na Khalifa, kwa namna fulani anafikia upamoja huu.

Rafiki zetu wapaswa kujaribu kadiri ya uwezo wao kukutana na Khalifa na wasiruhusu wazo hili kuingia moyoni mwao kwamba zawadi ya fedha ni lazima wakati wa kukutana au Baiat. Inaonekana kwamba wakina mama hawaambiwi habari hizi. Mara moja ilitokea kwamba wakati kikundi cha akina mama walipofanya Baiat, mwanamke mmoja alisimama na kuanza kumwambia mwenzake. Umefanya Baiat kwa nini hutoi zawadi ya fedha? Nilimsihi mara nyingi kwamba anapaswa kukaa chini kwa kuwa ni dhambi kusema meneno haya. Lakini aliendelea kusema; "Hii itakuwaje dhambi? Kutoa zawadi ya fedha ni lazima". Jambo kama hili halipaswi kutokea.

Nitapenda pia kuwaambia rafiki zetu wanaokuja kwenye mikutano kwamba kukata kucha ni Sunnah ya Kiislam, lakini nimeona kwamba watu wengi hawakati kucha zao vizuri. Mtu mmoja alipeana nami mkono na kucha zake zikanitoa damu. Sitasema kwamba msije kupeana nami mkono, na sitasema kwamba wakati wa kupeana mikono msiunyake mkono wangu kwa nguvu. Katika haraka inayokuwapo kunyaka mkono ndiko pekee kunakoweza kufanywa. Lakini nitasema kwamba mnapaswa kuzikata vyema kucha zenu ili nisiumie.

Imefasiriwa na Mussa A. Mpinga.

Msikiti wa Kwanza wa mjini Lindi

Kutoka uk. 1

Mwaka jana ujenzi wa Msikiti huo ulianzishwa ambapo Amirna Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib aliweka jiwe la msingi la Msikiti huo pamoja na watu wengi wakiwemo Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya. Katika sherehe hizo watu wafuatao waliweza kuweka matofali, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya, Mbashiri wa Mikoa ya Mtwara na Lindi - Shehikh Muhammad Afzal Bhatti (kwa sasa ni Mbashiri wa Mkoa wa Tanga), Sheikh Abid Mahmood Bhatti -Mbashiri wa Mkoa wa Ruvuma (kwa sasa ni Mbashiri wa mikoa ya Mtwara na Lindi), Bw. Muhammad Iqbal Dar mkazi wa Uingereza na Bw. Saidi Kalindima - Rais wa Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Ujenzi wa Msikiti huo uliendelea kufanyika hadi Octoba 2012, ambapo ukawa tayari kufunguliwa rasmi. Tarehe 23 Octoba 2012 Msikiti huo ulifunguliwa rasmi katika sherehe ya ufunguzi watu wapatao 150 wasiokuwa wa Ahmadiyya walishiriki akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Lindi pamoja na Wanajumuiyya wa Lindi na matawi mengine. Mkuu wa Wilaya aliyekuwa Mgeni Rasmi alifika kwa wakati na kushiriki katika mipango yote iliyojiri zaidi ya masaa mawili.

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania aliwakaribisha wageni wote na kutoa hotuba fupi, katika hotuba yake alieleza mafundisho ya mapenzi na amani ya Jumuiyya na kuwaambia kuhusu kauli mbiu ya Jumuiyya iliyo ni "Upendo kwa wote bila chuki kwa yeyote". Alisema ya kwamba "Kusudio hasa la kujenga msikiti ni kuwawezesha watu wafanye ibada ya Muumba wao na kwa kupitia Msikiti huu ujumbe wa Islam ulio ni ujumbe wa amani, mapenzi na upendo uwafikie watu wote, na Misikiti yote ya Jumuiyya inashughulikia madhumuni hayo. Aliendelea kusema; "Msikiti huu ambao tumejumuika hapa kuufungua rasmi milango yake iko wazi kwa watu wote. Kila anayependa kumwabudu Mwenyezi Mungu yuko huru kuingia na kufanya ibada humo".

Baadaye Amir sahib alimkaribisha mgeni rasmi aje kueleza machache. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliipongeza Jumuiyya na viongozi wake kwa kujenga Msikiti huu mzuri na kualikwa kwake katika hafla hiyo.

Mkuu wa Wilaya alisema ya kwamba "yeye anafahamu Jumuiyya tangu muda mrefu na anakiri ya kwamba Jumuiyya ya Ahmadiyya ni Jumuiyya ya amani na inapenda amani na kauli mbiu yake 'Upendo kwa wote bila chuki kwa yeyote' ni fundisho halisi la Islam na nimefarijika sana kwa kusikia ya kwamba Jumuiyya inashughulikia sana katika kufikisha ujumbe huu wa amani kwa watu wote na pia nimefurahi sana kwa kujua kwamba msikiti huu uko wazi kwa watu wote na nafanya maombi kwamba Msikiti huo uweze kuchangia mchango wake katika kutuunganisha kwa pamoja".

Kuna wanahabari walioshiriki katika hafla hiyo, walioendelea kurekodi na kuchukua picha za programu hii, na kurusha kwenye TV na redio na pia habari zingine zilipigwa chapa katika magazeti mbaimbali kama vile Redio TBC, TBC1, Chanel Ten, Redio Safari, Redio Clouds Dar FM, magazeti ya Kiingereza The Citizen, The Guardian na gazeti la Kiswahili Majira.

Msikiti huu umejengwa kwa kutumia Paundi elfu thelathini ambayo asilimia kubwa yaani Paundi elfu ishirini imetolewa na Bw. Muhammad Iqbal Dar wa Uingereza, Mwenyezi Mungu Ampatie malipo mema. Baadaye washiriki wote walialikwa kwenye tafrija iliyoandaliwa na Jumuiyya.

Ikumbukwe ya kwamba mji huu wa Lindi una historia yake maalum. Mwaka 1950 Mbashiri wetu Maulana Fazl Ilahi Bashiri alipofika hapa kwa Mahubiri, alipingwa vibaya na kurushiwa mawe na wakazi wa hapa na wengine walijaribu kumuua, hapo kabla haja ondoka alisema kwa watu hawa ya kwamba "Ninyi mmekadhibisha Imamu wa zama basi mtaona ghadhabu ya Allah ikishuka hapa, baada ya kutokea tukio hilo wiki moja haikupita kimbunga kimoja kilipita hapa kilicholeta madhara kwa hali ya juu. Wazee wa zamani wanakumbuka kimbunga kile mpaka leo. Na leo katika mji huu ujenzi wa Msikiti wa Jumuiyya ni ithibati ya ushindi wa Jumuiyya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

Wassalaam

Khalifa wa Islam atoa hotuba ya kihistoria katika bunge la Umoja wa Ulaya:

Kutoka uk. 1

Siku ya tarehe 4 Disemba 2012. Kiongozi Mkuu Duniani wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya na Khalifa wa tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alitoa hotuba ya kihistoria ya uzinduzi katika Bunge la umoja wa Ulaya huko Brussels mbele ya wasikilizaji waliojaza ukumbi wapatao takriban 350 wakiwa wageni wanaowakilisha nchi 30.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a, Khalifatul Masih V, akisalimiana na Dr. Charles Tannock MEP, Mwenyekiti wa taasisi ya 'Marafiki wa Waislam Ahmadiyya katika Bunge la umoja wa Ulaya'.

Wenyeji wa hafla hii walikuwa ni kundi lililoasisiwa karibuni 'Marafiki wa Waislam Ahmadiyya katika Bunge la umoja wa Ulaya', mwenyekiti wa kundi hilo na Manaibu wake wote walipanda jukwaani kumkaribisha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad. Martin Schulz Mbunge wa Bunge la Umoja wa Ulaya (MEP) na Rais wa Bunge la umoja wa Ulaya pia walijitokeza kumlaki Khalifa Mtukufu.

Katika hotuba yake iliyochukua takriban dakika thelathini na tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad aliutaka umoja wa Ulaya kuutunza umoja wao; akaongelea suala la ongezeko la uhamiaji katika nchi za Ulaya, akatoa wito wa kuwepo kwa umoja katika mahusiano ya kimataifa na akaongelea kwa kirefu juu ya mafundisho ya msingi ya Islam kuhusiana na kuleta amani Duniani.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alisema kwamba katika ulimwengu wa kisasa watu wengi wanaangalia Uislam kama Dini inayohamasisha machafuko na msimamo mkali na wanaulaumu kwa mengi ya machafuko yanayoendelea katika nchi mbalimbali za Duniani. Alisema kwamba tuhuma kama hizo kwa hakika si za haki ikizingatiwa kwamba "hata maana za neno lenyewe Islam ni amani na usalama"

Khalifa Mtukufu akazungumzia suala la wasiwasi ulioenea juu ya idadi ya wahamiaji katika nchi za Ulaya. Akitoa tathmini ya kina, Khalifa Mtukufu alisema suala hili linapelekea kwenye kuenea kwa 'wasiwasi na mashaka'. Khalifa Mtukufu aliwalaumu wote wahamiaji pamoja na wenyeji kuwa ni chanzo cha mtafaruku, ambapo wahamiaji wengi waliwachokoza wenyeji kwa kukataa kujichanganya, na kwa upande mwingine makundi fulani ya jamii wenyeji yalikuwa hayawataki wageni. Alisema matokeo ya mgawanyiko kama huo yanafika mbali na alizitaka pande zote husika kushirikiana kutatua masuala haya.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alisema; "Serikali zinahitaji kuunda sera ambazo zitathamini na kulinda heshima ya kila mmoja, ambazo kwazo kuumiza hisia za wengine au kuwasababishia wengine taabu ya aina yoyote kupigwe marufuku. Kuhusu wahamiaji, lazima waingie wakiwa na utayari wa kuchanganyika na wenyeji, vile vile wenyeji wawe tayari kufungua nyoyo zao na kuonyesha uvumilivu".

Kuhusu umoja wa Ulaya Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alisema; "Kuundwa kwa umoja wa Ulaya kumekuwa ni mafanikio makubwa kwa nchi za Ulaya, kwa kuwa kumekuwa ni njia ya kuunganisha bara la Ulaya. Na kwa hiyo yawapasa mfanye juhudi zote mnazoweza kuutunza umoja huu. Kumbukeni kwamba nguvu za Ulaya zimo katika kubakia kwake katika muungano kama kitu kimoja. Muungano kama huu hautakuwa wa manufaa kwenu ninyi hapa Ulaya pekee lakini katika ngazi ya Dunia utakuwa ni njia ya Bara hili kuhifadhi nguvu yake na ushawishi wake".

Khalifa alizungumza juu ya haja sio tu ya ushirikiano ndani ya Ulaya, bali alitoa wito wa muungano wa ulimwengu. Khalifa Mtukufu alisema; "Nikiongea kwa mtazamo wa Islam, tunapaswa kujitahidi ili ulimwengu mzima uungane pamoja. Katika suala la sarafu Dunia inapaswa kuungana katika suala la biashara na uchumi Dunia inapaswa kuungana. Na katika suala la uhuru wa kusafiri na uhamiaji, sera mwafaka na zinazotekelezeka zapaswa kuundwa, ili ulimwengu upate kuungana"

Khalifa Mtukufu alisema kwamba nchi za leo Duniani haziwezi tena kubakia katika utengano na hata nguvu kubwa za Dunia kama Marekani zinategemea biashara za kimataifa na uhusiano na nchi za nje.

Alisema nchi zilizoendelea hazipaswi kuzinyonya nchi maskini ila zizisaidie ili zipate maendeleo na mafanikio. Hadhrat Mirza Masroor Ahmad vilevile aliongelea suala la migogoro katika ulimwengu wa Kiarabu na Mashariki ya Kati. Alisema kwamba kile ambacho ulimwengu wa Magharibi umekieleza wazi wazi 'kuchukizwa na kuguswa' kuhusiana na hali za Syria na Libya, hawakuelekea kuguswa kwa namna hiyo hiyo na kadhia ya watu wa Palestina.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alisema; "Hali hii inayoonekana ya viwango dufu inasababisha manung'uniko na chuki kuongezeka katika nyoyo za watu kwenye nchi za Kiislam dhidi ya nchi kubwa za Dunia. Hasira hii na uadui ni vya hatari sana na vyaweza kuchemka na kulipuka wakati wowote. Na iwe wazi kwamba siongei kwa kuunga mkono au kulinda maslahi ya nchi moja wapo iwayo yoyote. Ninachotaka kusema ni kwamba aina zote za ukatili, popote zilipo ni lazima zondoshwe na kusitishwa, bila kujali kama zinafanywa na watu wa Palestina, watu wa Israel au watu wa nchi yoyote nyingine"

Khalifa pia aliilaumu kanuni ya nguvu ya Veto ndani ya Taasisi za kimataifa. Alisema kwamba historia ya upigaji kura ya wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la umoja wa mataifa inaonyesha kwamba katika matukio fulani nguvu ya Veto ilitumiwa vibaya ili kuusaidia ukatili, badala ya kuuzuia.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alihitimisha hotuba yake kwa kutoa wito wa haki na usawa, alisema; "Daima kumbukeni kwamba amani yaweza tu kupatikana kwa kuwasaidia wote, wakandamizwaji na wakandamizaji kwa namna ambayo haitapendelea upande wowote, kwa namna isiyogubikwa na tamaa za kisirisiri na isiyokuwa na chuki yoyote. Amani huundwa kwa kuzipa pande zote jukwaa lililo sawa na uwanja wa aina moja wa kuchezea".

Kabla ya hotuba ya uzinduzi (MEPs) wabunge kadhaa wa Bunge la umoja wa Ulaya walipanda jukwaani na kuzungumzia kupendezwa kwao na Islam ya amani kama inavyoelezwa na Jumuiyya ya Waislam Ahmadiyya.

Dr. Charles Tannock (MEP), Mwenyekiti wa kikundi cha wabunge wa umoja wa Ulaya Rafiki wa Islam Ahmadiyya alisema kwamba; "Waislam wa Ahmadiyya ni mfano unaohitajika wa ustahimilivu ulimwenguni! Alilaani mateso dhidi ya Waahmadiyya huko Pakistani na kusema 'Kauli mbiu ya Ahmadiyya ya Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote ndiyo dawa dhidi ya wenye msimamo mkali na wanajihadi'.

Tunne Kelam (MEP), Naibu Mwenyekiti wa kundi la Marafiki wa Waislam wa Ahmadiyya katika Bunge la Umoja wa Ulaya, alisema; yeye binafsi alikuwa anahudhuria tukio hili kwa sababu ilikuwa ni fursa ya kujiunga katika juhudi ya kuleta amani! Aliisifu Jumuiyya ya Waislam Ahmadiyya kwa kukataa vurugu zozote na ugaidi' na akaapa kuisaidia Jamaat ulimwenguni pote.

Baroness Sarah Ludford (MEP), Naibu Mwenyekiti wa kundi la Marafiki wa Waislam wa Ahmadiyya katika Bunge la Umoja wa Ulaya, alizungumzia uhusiano wake wa muda mrefu na Jumuiyya ya Waislam Ahmadiyya huko (Uingereza). Akasema kwamba kauli mbiu ya Jamaat ilikuwa ni uamsho ambao ulikuwa unahitajika sana katika ulimwengu wa kisasa.

Claude Moraes (MEP) Naibu Mwenyekiti wa kundi la Marafiki wa Waislam wa Ahmadiyya katika Bunge la Umoja wa Ulaya, alisema kwamba hafla hii imewavutia wahudhuriaji wengi zaidi kuliko inavyotokea katika kikao chochote cha Bunge la Umoja wa Ulaya.

Jeen Lambert (MEP), Mwenyekiti wa Tume ya umoja wa Ulaya kuhusu Asia ya kusini, alisema kwamba atafuatilia katika Serikali ya Pakistan suala la haki ya kupiga kura ya Waislam wa Ahmadiyya. Alisema kwamba ilikuwa ni lazima pande zote ziwe na haki sawa ya upigaji kura kwa uhuru na bila ubaguzi.

Rais wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Uingereza Bwana Rafiq Hayat, alipanda jukwaani kueleza kufurahishwa kwake kwa kuasisiwa kwa 'kikundi cha Marafiki wa Waislam Ahmadiyya katika Bunge la Umoja wa Ulaya".

Hafla hii ya kihistoria ilihitimishwa saa 10:35 jioni (saa za Ulaya) kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Hadhrat Mirza Masroor Ahmad.

Habari zaidi; press@ahmadiyya.org.uk

Umuhimu wa Elimu katika Islam

Hotuba iliyotolewa na Sheikh Asif Butt katika Jalsa salana 2012.

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu.

Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Alimwumba mwanadamu kwa tone la damu lililoganda. Soma !na Mola wako ni mbora kuliko wote. Ambaye alifundisha kwa kalamu. Alimfundisha mwanadamu yale aliyokuwa hayajui.

(sura : 96 aya :2_6)

Awali ya yote, sina budi kumtolea shuQur'an nyingi Mungu Mwenye Enzi ambaye kwa fadhila na rehema zake zisizohesabika ametuwezesha kwa mara nyingine tena kuhudhuria mkutano huu wa mwaka wenye baraka kemkemu ili tuweze kujisafisha na kujitakasa nafsi zetu kwa kujipatia chakula cha kiroho kinachogawanywa katika kipindi hiki cha siku tatu. Ndugu wasikilizaji, kama mlivyosikia, mada ya hutuba yangu ya leo ni "*umuhimu wa taalimu kwa watoto na wajibu wa wazazi katika malezi yao*".

Miaka elfu moja na mia nne iliyopita kabla ya leo, kulikuwa na wakati ambapo watu wa dunia nzima walikuwa wamezama katika giza totoro za ujahili na maasi, ndipo nuru moja ilishuka kutoka mbinguni na jua la elimu lilichomoza kwa nguvu zake zote kiasi hiki kwamba liliondolea mbali giza za kila namna. Kwa hakika jua hili lilikuwa ni uislamu uliowatoa waarabu katika shimo refu la ujinga na ujahili. Bara arabu lile lile lililokuwa kituo cha uasi, uovu na ujinga, likageuka kuwa kitovu cha elimu na hekima. Mabedui wale wale waliokuwa hawazitambui asilani khulka ndogo ndogo za kawaida, wakawa waalimu wa kufundisha khulka kubwa kubwa. Basi mafuriko haya ya elimu yaliendelea kuzagaa na kusambaa kila upande na kuwapamba watu wa ulimwengu mzima kwa mapambo ya elimu na khulka njema. Na baadaye ulifika wakati ambapo taa hii ya elimu ilikuwa mikononi mwa waislamu tu na wengine wote walikuwa wamezama vibaya ndani ya giza za ujahili.

Karne chache zilizopita, huku ulaya asilimia tisini ya watu walikuwa hawajui kusoma wala kuandika wakati katika nchi za kiislam asilimia tisini ya watu walikuwa wanajua kusoma na kuandika. Lakini sawa na utabiri wa Mtume wetu Mtukufu s.a.w. hali hii ikabadilika kabisa na baadaye kwa bahati mbaya waislamu walimsahau Mola wao na mafundisho yake na wakabakia kuwa waislamu wa jina tu na polepole wakaendelea kuwa mbali na elimu kiasi kwamba ujinga wa kila namna ulinasibishwa kwao.

Wasikilizaji watukufu, kwa mujibu wa bishara za mkweli wa wakweli wote s.a.w, hali hii ilikuwa lazima iwapate waislamu lakini hali hiyo isingeweza kudumu kwa muda mrefu sana kwani nuru ya Islam ilikuwa ing'ae kwa mara nyingine tena na habari za jua hili la elimu kutokeza mara ya pili kwa shani yake yote, zilitoleawa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake s.a.w. Lakini haya yote yalikadiriwa kutokea wakati wa ujio wa mara ya pili ya Mtume Muhammad s.a.w. yaani katika zama za Masihi na Mahdi aliyeahidiwa a.s. Na kwa kumpitia huyu Masihi na Mahdi a.s, taa hii ya elimu ilikuwa iwashwe tena na kuwaangaza watu wa dunia nzima naye alikuwa aje kububujisha chemchem za elimu na maarifa na kuwagawia watu hazina hizi za kimbinguni.

Wasikilizaji wapenzi, zama hizi tukufu za huyu Masihi na Mahdi zimekwisha wadia tayari na yule Masihi wa Muhammad s.a.w aliyetabiriwa kuja, amekwisha wasili na kugawa hazina hizi za kielimu zisizoweza kuisha mpaka siku ya kiyama.

" wo khazain jo hazaruun saal se madfuun the Ab men detu hun ager koi mile ummeed waar"

"Hazina zile zilizokuwazimefichikakwa karne nyingisana, sasa nazigawa hizo kama kuna ye yote mwenye kuzitamani"

Kisha akiwapa habari ya furaha wafuasi wake, Sayyedena Ahmed a.s alisema " *mere firka ke log iskadar elam aur maarifat men kamaal hasil karen ge ke apne sachai ke noor aur dalael aur nishanun ki ruu se sab ka mun band kar den ge."* (tajjaliyyate ilahiya ,17)

Yaani wafuasi wangu watapata ukamilifu katika medani ya elimu na maarifa kiasi hiki kwamba kutokana na nuru yao ya ukweli, dalili na ishara wataifumba midomo ya watu wote.

Enyi matawi mabichi ya mti wa dhati ya Masihi wa Muhammad s.a.w, hongera sana kwenu kwamba mmejaaliwa kuzipata zama hizo tukufu ambazo mamilioni ya watu wamekata roho wakitamani kuzipata na kuziona zama hizo. Lakini hamwezi kamwe kuzifikia na kuzipata hazina hizi zilizotolewa na Sayyedena Ahmad a.s katika zama hizi za mwisho mpaka mtekeleze majukumu na waibu wenu barabbara. Na wajibu wenu wa kwanza kabisa ni kuwalea watoto wenu kwa malezi bora, mkiyatanguliza matendo yenu mema, maana watoto wa leo ni taifa la kesho. Mwenyezi Mungu ananena ndani ya Qur'an Tukufu: *"Enyi mlioamini ! jiokoeni nafsi zenu na ahali zenu*



Sheikh Asif Mahmood Butt

katika moto ambao kuni zake ni watu na mawe" (Sura: 66:6)

Mtume wetu Mtukufu s.a.w alisema "enyi watu kila mmoja wenu ni msimamizi na ataulizwa na Mwenyezi Mungu kuhusu alivyowatendea wale waliokuwa chini ya usimamizi wake." Masihi na Mahdi aliyeahidiwa, Sayyedena Ahmad a.s alisema "watu wanatamani sana mno kupata watoto, na wanapata pia watoto, lakini haikutazamwa kwamba wanafanya mipango na jitihada kwa ajili ya malezi, adabu na mwenendo mwema wa watoto wao ili wawe watiifu mbele ya Mwenyezi Mungu. Hawawaombei katu watoto wao wala hawazingatii taratibu za malezi yao."(Malfuzat, Jal:1, uku: 562)

Kwa hiyo, ndugu wasikilizaji, kulingana na maagizo hayo yaliyotolewa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake , wajibu mkuu wa wazazi ni kuwalea watoto wao vizuri katika maadili mazuri na mtu asitamani tu kujaaliwa watoto bali baada ya kupata watoto afanye kila liwezekanalo kuwafundisha tabia njema na khulka nzuri na kuwaelimisha sawa sawa kama wasemavyo waswahili "kuzaa sio kazi bali kulea ndiyo kazi." Na Mtume wetu Mtukufu s.a.w. akiwahimiza na kuwahamasisha wazazi kuwalea watoto vizuri, alisema kuwa zawadi bora kabisa ambayo baba anaweza kumpatia mwanae ni malezi mema tu. Na kwa ajili ya malezi mazuri ya mtoto, Mtume s.a.w alifundisha kuomba maombi maalum mwanzoni tu mwa mahusiano ya kindoa. Dua hii ni ya kuepushwa na nguvu za kishetaniyaaniendapouhusiano wao utajaaliwa kupata kizazi, basi kizazi hicho kiepushwe na shetani. Mtume s.a.w alisema "mmoja wenu anapokutana na mke wake basi aombe kuwa E Mola wetu tuepushe na shetani na mtoto huyu utakayetujaalia naye pia mwepushe na shetani. Wakijaaliwa kupata mtoto bila shaka yo yote ataepukana na shetani. Dua hii ikiombwa wakati wa heka heka hizi , huonesha kuwa waaminio wamemtanguliza Mwenyezi Mungu kwa mategemeo na mapenzi makubwa. Kwa hiyo, bila shaka maombi yao haya hupokelewa na Mwenyezi Mungu na matunda yanayopatikana huwa ni mazuri tu. Kisha mtoto anayezaliwa katika dini ya asili anatakiwa asikie sauti ya haki ndiyo maana Mtume s.a.w. aliagiza kwamba adhana itolewe katika sikio lake la kulia na iqama itolewe katika sikio lake la kushoto ili ionekane kana kwamba mtoto amekwisha anza maisha ya vitendo na kwamba sasa wazazi wake wanapaswa waandae mipango ya malezi yake.

Kitu kingine kilicho muhimu sana kwa ajili ya malezi ya mtoto ni kumpa jina zuri. Inasikitisha na kuhuzunisha sana kwamba siku hizi watu wengi sana hawaijali desturi hii ambayo kwa hakika nisunna ya Mtume wetu Mtukufu s.a.w naye alisema " wapeni watoto wenu majina ya manabii , Mwenyezi Mungu anapenda sana majina ya Abdullah, Abdurahmaan, vile vile Haarith na Hamaan. Kuwapa watoto majina, pia kuzingatie taratibu za malezi yao kuwa wazazi wanapowapa watoto wao majina, wajue na kuzingatia kwamba wanamwandaa mtoto awe na sifa ya jina analopewa na sifa za kuwa Abdu yaani mtumishi wa kweli wa Mwenyezi Mungu, zipandikizwe. Majina wanayopewa yaoneshe wema ndani yake na pia yawe na maana nzuri, yasioneshe udhalilifu na chuki ndani yake. Zama za uhai wa Mtume s.a.w. endapo mtu alimpa mtoto jina lisilo na maana yoyote nzuri, Mtume s.a.w alilibadilisha jina hilo na kumpatia mtoto jina jingine lenye maana nzuri kwani jina analopewa mtoto huathiri sana mwenendo wake pia. Hivyo basi, twapaswa kuzingatia sana maagizo haya ya Mtume s.a.w na kubadilisha mara moja majina yasiyo na maana nzuri na alhamdu lillah katika jumuiyya ya waislamu waahmadiyya kuna desturi nzuri ya kumwomba Khalifa wa wakati kumpa mtoto jina. Kwa kuifuata desturi hii, wanajumuiyya si tu kwamba wanapata jina zuri kwa mtoto wao bali wanafaidika na baraka na maombi ya khalifa wa wakati.

Wasikilizaji waheshimiwa, wako watu wengi ambao wanachangia kwa kiasi kikubwa katika kuwaharibu watoto wao wenyewe, na hao ni wale wanaowaacha watoto wao huru wafanye wayapendayo, kwa madai ya kwamba watoto ni watoto tu lakini watu hao hawaelevi kwamba malezi ya mtoto huanza mara baada ya mtoto kuzaaliwa. Maana muda bora kwa malezi ni muda wa utotoni. Safari moja mjkuu wa Mtume s.a.w Hazrat Hasan r.a aliyekuwa mtoto mdogo wakati huu, alichukua tende moja katika tende za sadaka na kuweka kinywani mwake, Mtume s.a.w aliyekuwa anamtazama, mara moja akatia kidole chake kinywani mwa Hazrat Hasan r.a. na kuitoa ile tende kwa kumwambia kuwa tende za sadaka ni haramu kwako kuzila. Tukio hili kidhahiri linaonekana dogo lakini kimalezi na kimaadili ni kubwa mno, hata waswahili wasema "mkunje samaki yungali mbichi". Mwanzilishi Mtukufu wa dini ya kiislam, Mtume Muhammad s.a.w, wakati mmoja alisema "hakuna mtoto yeyote isipokuwa huzaliwa katika asili sahihi (ya kiislam), wazazi wake ndio humfanya myahudi, mkristo, au mmajusi." Kauli hii ya Mtume s.a.w inawaelekeza wazazi wazingatie jambo hili kuwa kila mtoto huzaliwa katika asili sahihi ya kiislam na anapokuja duniani, ubongo na mawazo yake huwa ni safi kama karatasi nyeupe isiyoandikwa cho chote. Inapaswa kuangalia sana kwamba ubongo huu ulio safi, usipate athari mbaya za mazingira mabaya. Ni lazima sana kuanza kumwelimisha mtoto mara tu anapoanza kupata fahamu kwani nuru ya elimu huunoa ubongo wa mtoto na kwa kutumia elimu anaweza kupamabanua baya na zuri. Matukio mengi hujulikana kwa sababu ya elimu, na elimu humfanya atofautishe baina ya njia sahihi na njia potovo, ajifunze mema na njia ya kupata maendeleo. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu ameipa elimu umuhimu mkubwa ndani ya Qur'an Tukufu kama asemavyo

"*Sema, je* wanaweza *kuwa sawa wale wenye elimu na wasio* na *elimu? wenye akili tu hushika mawaidha.* (sura : Az-zumar, aya : 10)

Tena umuhimu wa elimu unadhihirika kutokana na amri ya Mwenyezi Mungu aliyomwamuru Mtume wake Muhammad sa.w *"kul rabbe zidni ilmaa"* yaani E Mola wangu nizidishie elimu. Tafakarini kwa muda mfupi tu juu ya jambo hili kwamba mpendwa wa Mwenyezi Mungu, fahari ya manabii, aliyeleta sheria iliyojikusanyia kheri zote na elimu zote, anaamrishwa kuomba dua ya kujiongezea elimu. Sasa sisi tulio watu wa kawaida tunapaswa kujitahidi namna gani kuitafuta elimu, kila mmoja anaweza kulielewa hilo kwa urahisi. Mtume Muhammad s.a.w alisema "kutafuta na kujifunza elimu ni faradhi juu ya kila mwislamu mwanamume na mwanamke. Kisha akasema kuwa mwanzo wa kujifunza elimu ni utotoni, na "*mathalullazi yata'allamul ilma fii sighrehi kannakshe alal hijre"* yaani mfano wa ajifunzaye elimu utotoni mwake ni kama nakshi iliyo juu ya jiwe.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Mwalimu Rashid Mussa Ungando hatunaye

Na Mahmood Hamsin Mubiru
- Dar es salaam

Majira ya saa 12:15 asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 21 kuamkia 22 mwezi wa kumi na moja 2012, kama ilivyo desturi yangu nilikuwa nasikiliza kipindi cha 'Amka na BBC' na mara nilisikia simu ikiita. Nilipokea simu hiyo kutoka kwa Bwana Ahmad Bishazo ambaye baada ya Assalaam Alaikum aliniuliza; "Je umepata habari?". Nikamuuliza "Habari gani?". Akasema "Mwalimu Rashidi Mussa Ungando amefariki". Kwa sauti ya masikitiko nilimueleza; "*Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea*".



Mwalim Rashid Mussa Ungando aliyefariki akiwa na umri wa miaka tisiiniwake

Mwalimu Rashidi Mussa Ungando tulijuana sana, labda kwa sababu ya kufanya kazi moja ya Ualimu. Alikuwa ni mpole na ilikuwa kwa nadra kumkuta anazungumza. Akifika Msikitini anajikalia pembeni kabisa na huku akimkumbuka Mola wake. Nilipopata habari tu ya kwamba amejiunga na Jumuiyya katika miaka ya hamsini (50) nilipata hamu sana ya kuzungumza naye ili anipatie taswira ya hali ya Jumuiyya ilivyokuwa katika miaka hiyo. Nilifunga safari hadi Kibiti ambako kwa bahati mbaya sikukutana naye. Kabla sijaondoka nyumbani kwake, nilimuachia ujumbe ili aweze kunieleza historia yake kwa ufupi kuhusu alivyo jiunga na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Wiki moja baadaye nakumbuka ilikuwa ni siku ya Ijumaa nilimuona amekumbatia furushi na katika furushi hilo kulikuwepo na vitu vya zamani kuhusu Jumuiyya yakiwemo magazeti ya East African Times. Litakumbukwa ya kwamba gazeti hili katika lugha ya Kingereza lilianzishwa na Maulana Sheikh Mubaraka Ahmad ili kuwafikishia ujumbe wale ambao hawafahamu Kiswahili.

Mwalimu Rashidi Mussa Ungando alikuwa ni hodari sana wa kutunza vitu vya zamani tena katika mpangilio unaoonesha umakini aliokuwa nao. Karatasi zake nyingi zinazohusu Jamaat, zikiwemo habari za Ahmadiyya, barua mbalimbali kutoka kwa Masheikh na wale aliokuwa anajaribu kuwahubiri zote hizo zilitunzwa kwa uangalifu mkubwa. Na katika zawadi adhimu aliyokuja nayo katika furushi lile ni utimizaji wa ombi langu la kunieleza jinsi alivyojiunga na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Andiko hili limejaa mambo mengi ya historia ambayo yatatusaidia kufahamu hali ilivyokuwa wakati huo katika miaka ya 50. Makala hiyo ameipa kichwa cha maneno 'BARABARA KUELEKEA JUMUIYYA AHMADIYYA KUTOKA 1943 - Rashidi Mussa Ungando'.

Umati uliomiminika katika mazishi ya marehemu Rashidi Mussa Ungando yaliyofanyika makaburi ya Waahmadiyya Wailes - Temeke tarehe 22/11/2012 na maelezo yaliyotolewa na wale waliokuwa wanafunzi wake na waliomfahamu ni ushahidi wa wema wa Mwalimu huyu ambaye wanafunzi wengi wamepitia mikononi mwake. Watu wengi walijitokeza siku ya mazishi kumuaga Mwalimu wetu na hao wote walimmiminia sifa tele kuhusu upole wake na taadhima. Wazee kadhaa walisimama na kukiri ya kwamba elimu waliyoipata na adabu aliyowafundisha ni vitu ambavyo vimewasaidia katika maisha yao.

Mwalimu Ungando kama makala yake tuliyoitaja hapo juu ilivyoonesha alipenda na kuthamini sana elimu, na moja ya chimbuko kubwa la elimu ni vitabu. Alijijengea utamaduni wa kupenda kusoma na bila shaka mapenzi yake kwa kusoma yana mchango kuhusu kujiunga kwake na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Utamaduni huu kwa bahati mbaya kwa hivi sasa umetoweka na kumeliletea taifa letu hasara kubwa.

Wakati wote toka ajiunge na Jumuiyya ya Ahmadiyya mwaka 1956 Mwalimu Rashidi Mussa Ungando alitanguliza dini mbele ya kila kitu. Wale wote waliokuwa karibu naye walifahamu fika itikadi yake. Itikadi yake ilijitokeza vyema katika khulka na mwenendo wake. Nyumba yake kule Kibiti ilifanywa mahala pa kusalia na hii hapa ya Dar es salaam (Wailes nyumba No. 8) palikuwa ni mahala ambapo ile bughudha kwa wapangaji haikuweza kupatikana. Tabia yake ilijitokeza vizuri zaidi kutokana na nyumba yake iliyopo mjini Dar es salaam.

Kabla ya kueleza tukio hili kuhusu nyumba yake ya Wailes Temeke ni vizuri kueleza mikasa na vitimbwi vinavyohusu wenye nyumba katika jiji hili.

Kupanga nyumba katika jiji la Dar es salaam kuna adha na machungu yake. Kama hujaoa hiyo nayo ni nongwa hupati chumba. Hawajali kufahamu sababu ambazo zimekufanya kuwa bado hujaoa. Ukijaliwa kupata chumba ipo mikataba ya aina mbili, kulipa kodi kila mwisho wa mwezi au kulipa kodi ya mwaka mzima. Na kama ni malipo ya kila mwezi baba au mwenye nyumba asubuhi kabla jogoo hajawika yuko mlangoni kutaka kodi yake. Nisikilizie yatakayotoka mdomoni kama hujabahatika kupata kodi yake! Na ukilipa mwaka anaimaliza na mara kwa mara anataka mkopo na kusema tutajuana katika kodi ya mwaka ujao. Tazama kivumbi kama umejaaliwa watoto, utamsikia watoto gani hawa! Mtanivunjia milango yangu! Ukipata wageni, wageni humu ndani hawaishi! Mtatujazia choo. Basi fanya kosa la kukaanga wakati bado hujalipa kodi yake. Maneno yatakayotoka pale la haula!. Ukichelewa kidogo tu kurudi nyumbani utakiona chamtema kuni, kwani hautafunguliwa mlango abadani ama utapewa maneno ambayo hutayasahau. Mtu akijaliwa kujenga nyumba yake anatakiwa ainue mikono kumshukuru Mungu.

Mwalimu Rashidi Mussa Ungando alikuwa ni Baba mwenye nyumba wa aina yake. Na ushahidi umetolewa na wale walioishi katika nyumba yake iliyopo Wailes nyumba Namba 8. Mwalimu Omari Mnungu ameishi katika nyumba hiyo takribani miaka minane. Anasimuliakuwakilaaliyekuwa katika nyumba hiyo alitoka kwenda kwenye nyumba yake au aliyotayarishiwa na Taasisi yake. Hata siku moja hakuomba kodi. Ilikuwa ni wajibu wa mpangaji kuwasilisha pesa hizo kwake. Wakati wa mazishi yake wapangaji wake wa zamani walikuwepo kwa wingi, kwani waliishi katika nyumba hiyo kwa wema na kuondoka kwa wema. Mlango wa nyuma wa nyumba yake aliamuru ubaki wazi usiku kucha ili kuwasaidia wale waliochelewa kurudi kutoka kwenye mahangaiko ya maisha. Wengine hata miaka mingi baadaye walipoenda kumtembelea katika nyumba yake ile na kumkosa walifunga safari hadi Kibiti - alikokuwa amehamia ili kumjulia hali.

Kiwango chake cha uvumilivu kilikuwa ni cha hali ya juu. Mpangaji mmoja alifurutuada. Yeye alikuwa mlevi wa kutupwa na kujisaidia humo humo ndani. Mwalimu Rashidi Mussa Ungando hakuwahi kutoa hata neno moja la kumkaripia mpangaji huyo. Lakini sifa hizo nadhani inabidi ziwaendee pia wake zake ambao nao walionesha uvumilivu wa hali ya juu mno na hii bila shaka ni kutokaana na kuathiriwa na mafundisho mazuri ya Jamaat Ahmadiyya.

Wenye nyumba wanalo la kujifunza kutoka kwa Mwalimu Rashidi Mussa Ungando. Nyumba na mali zozote tunazoruzukiwa ni mapambo ya dunia, ni maua ambayo uzuri wote mwisho ni kunyauka. Hili alilifahamu Mwalimu Rashidi Mussa Ungando na akalitekeleza kwa vitendo.

Labda hatutakosea tukisema ya kwamba Mwalimu Rashidi Mussa Ungando amekuwa miongonni mwa Walimu wa zamani ambao raha yao yote ilikuwa ni kutoa elimu kwa mapenzi na huba kubwa sana. Ni miongoni mwa Walimu ambao kwa wajihi na tabia waliweza kuwa na mvuto na kuwafanya wanafunzi wake waige mwenendo wake. Wapo walioiga sauti yake, wapo walioiga pia jinsi alivyokuwa akitembea. Hii ni alama ya athari ya Mwalimu kwa mwanafunzi.

Kila mwanafunzi alipokosea alimwambia kosa lake, na kila alipofanya vyema alipata zawadi. Ukiona mwanafunzi amemfuata Mwalimu wake baada ya miaka 20/30 kupita basi uelewe mwalimu huyo alikuwa na mvuto wa ajabu uliotoa taswira ya khulka yake njema.

Walimu wa Ki-Ahmadiyya ametuachia mfano wa kuiga na sote ametukumbusha maneno ya Shaabani Robert katika 'Adili na nduguze' "Maisha ni safari na dunia ni matembezi kwa binadamu. Maskani yao ya milele yapo peponi. Hapana mtu ambaye atabaki duniani". Hapana shaka Sheikh Shaaban Robert amechota kwenye Qurani Tukufu Mwenyezi Mungu Anaposema - ***Kullu Nafsi dhaaikatul mauut,*** Kila nafsi itaonja mauti.

Bismillahir Rahmaanir Rahiim

SHULE YA SEKONDARI - AHMADIYYA KITONGA

NAFASI ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2013

Kamati ya Shule ya Sekondari - Ahmadiyya Kitonga, inapenda kuwatangazia Wanajumuiya na wananchi kwa ujumla kwamba nafasi kwa ajili ya kujiunga na kidato cha kwanza 2013 bado zipo.
Ada ya shule kwa mwaka ni *Tsh. 400,000/- kwa wanafunzi wa kutwa na *Tsh. 800,000/- kwa wanafunzi wa hosteli.
Wanafunzi wanaotaka kujiunga na kidato cha kwanza 2013 wanatakiwa wachukue fomu shuleni Kitonga Dar es Salaam au Makao makuu ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Mnazi Mmoja Dar es Salaam.
Wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga watatakiwa walipe theluthi mbili ya malipo yote kabla ya kuanza kwa masomo.
Wanafunzi wa kutwa watalipa: Tsh. 260,000/- kwa muhula wa kwanza
Wanafunzi wa hosteli watalipa: Tsh. 520,000/- kwa muhula wa kwanza
Malipo yatakayobaki yatalipwa kabla ya kuanza kwa muhula wa pili.

Wahi mapema, nafasi zilizobaki ni chache.

(Sare za shule, madaftari na vifaa vingine vya matumizi ya kawaida ya mwanafunzi havijajumuishwa katika malipo haya, taarifa zake zinapatikana kwenye fomu ya kujiunga na shule)

Kwa mawasiliano: 0655-105096; 0773-105096, 0684-105096; 0763-756396

Bustani ya Washairi

KWAHERI WETU MWALIMU

Bismillahi Kahari, Muumbaji wa sayari
Alomtuma Bashiri, Kutuletea khabari

Kutuletea khabari, Za kuepuka na nari
Na mambo yote ya shari, Tukatupa kwa kijiti

Tukatupa kwa kijiti, Mambo yenye tashtiti
Tukashika hasanati, Yote uloagizia

Yote uloagizia, Ni mengi tena mamia
Moja lililozidia, Masihi Muahidiwa

Masihi Muahidiwa, Vyovyote takavyokuwa
Duniani akitua, Lazima kumpokea

Lazima kumpokea, Ametoka kwa Jalia
Muumbaji wa dunia, Kheri utajipatia

Kheri utajipatia, Masihi kumpokea
Ungando hakubakia, Haraka kumpokea

Hivi leo katawafu, Amerudi kwa Raufu
Rashidi mwana nadhifu, Huzuni kubwa ajabu

Huzuni kubwa ajabu, Katuondoka Habibu
Mwalimu wetu muhibu, Rashidi Mussa Ungando

Rashidi Mussa Ungando, Kawapa wengi uhondo
Akija Juma na Kondo, Elimu kujipatia

Elimu kujipatia, Na mengi kujipatia
Yanayohusu dunia, Na akhera kadhalika

Na akhera kadhalika, Katu hakughafirika
Masihi ameshafika, Hakusita kuwambia

Hakusita kuwambia, Mtume wetu Nabia
Mwisho wake wa sheria, Siyo mwisho wa utume

Siyo mwisho wa utume, Watakuja wanaume
Waje kuwasha umeme, Gizani kutuondoa

Gizani kutuondoa, Ameshafika Rasua
Kaanzisha Jumuia, Yaitwa Ahmadia

Yaitwa Ahmadia, Kwa amri ya Jalia
Imekuja tukomboa, Nuru kutuangazia

Nuru kutuangazia, Na mengi kuelezea
Yale ya kutufufua, La kwanza Kuruani

Cha kwanza kutanguliza, Ni kitabu cha Muweza
Na yote kuyatimiza, Yote Alotuambia

Yote Alotuambia, Mfano kufa Nabia
Kafia kule India, Issa mwana Mariamu

Issa mwana Mariamu, Elewa enyi kaumu
Kazikwa yuko kuizmu, Hatorudi asilani

Hatorudi asilani, Kuja tena duniani
Ila mfano makini, Ghulamu wa Qadiani

Ghulamu wa Qadiani, Ni Mtume wa Manani
Na kila ano amini, Kumpokea wajibu

Kazi ameitimiza, Yarabi Mola Muweza
Yote yanayoumiza, Baidi yasimfike

Kaditamati wa tama, Rabbana mpe salama
Ili apate uzima, Ule tuloahidiwa.

Mahmood Hamsin
Mubiru (Wamamba), Dar es salaam

HOJA ZETU

1. Hawa wapinzani wetu, si watu watadaburi,
   Tutowapo hoja zetu, kwa Aya na mistari,
   Mbele yetu huwa butu, Mikuki hata khanjari
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua.
2. Wale waliothubutu, kujipanua suduri,
   Kutoka mbele za watu, pasi na kuwa jasiri,
   Walitafuta fukutu, wapate kujisitiri,
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
3. Twawakumbusha wenzetu, watumie tafakuri,
   Wazipime hoja zetu, na maneno ya Kahari,
   Islamu zamu yetu, Mahadi amedhihiri
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
4. Masihi kwao wenzetu, eti si habari nzuri,
   Issa kuwa kati yetu, eti hiyo ni hatari,
   Hadhi ya Mtume wetu, itachimbiwa kaburi
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
5. Nabii Issa ni wetu,hili kasema Rasuli,
   Kaja kazaliwa kwetu, kwa mara hii ya pili,
   Inakuwaje wenzetu hili hamlikubali
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
6. Issa wa kwanza ni mfu, Kuruani yakariri,
   Siku nyingi katawafu, amelala Kashmiri,
   Naye yumo kwe safu, ufufuo asubiri,
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
7. Siku tukufu laili, walishuka Masayidi,
   Jamii ya Marasuli, kwenye ile Masjidi
   Walishuka wakasali, nyuma yake Muhammadi
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
8. Kisa kile cha Isra, kadhalika na Miraji
   Ndaniye kina Ibura, someni sura Buruji,
   Muone dini Kinara, na mtume Mfariji,
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
9. Safari ya Jibrili, na mtume Muhammadi,
   Katika mbingu ya pili, lssa kapigiwa hodi,
   Hapo kwa wenye akili, kifoche ni ushahidi
   Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
10. Aridhi yetu kifata, makao yetu Dahari,
    Ah'yau amuwata, sote inatusitiri,
    Vipi Issa alipata, kugeuza desturi,
    Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
11. Mtakaa mtasota, kushuka Issa si kweli
    Siku tele zitapita, hamtaliona hili,
    Mikila bado navuta, hoja yataka akili
    Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua
12. Hapa naweka nukta, wa Msata na Kongowe
    Hoja hii yawasuta, acheni kupiga yowe,
    Wapi Aya mtapata, asaa iwaokowe,
    Hoja zetu madhubuti, nani wakuzipangua

Abdulrahman Mikila (Siasa), Morogoro

WENYE MFUNDO MADOBI - ZIFUWENI NYOYO ZENU

1. Tumeundiwa muundo, na Islam zamani
   Kukumbushana matendo, Anayotaka Manani
   Na tahadhari ya pindo, ya yale Asotamani
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
2. Basi napiga mdundo, si wa ngoma ni maghani
   Siyo ya kikafirondo, ni ya kuwamo kundini
   Kundini humo mwa mwendo, Allah Alioidhini
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
3. Ewe Mola wa upendo, Mwenye enzi Rahmani
   Nimejipandisha pando, na mzigo wa fulani
   Nafunga kwenye jamando, huu hapa mkononi
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
4. Safari yetu ya pendo, ya kumpenda Affani
   Ndanimwehumomwanyendo,kunamingimitihani
   Tudande vyema midando, tusianguke njiani
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
5. Kila Nafsi ya Fundo, ina kubwa walakini
   Inagandisha migando, ya mema ya Muumini
   Usiwe na huo mwendo, huwi mmoja peponi
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
6. Fundo sumu ya Mwenendo, safari ya shaitwani
   Nayo hutia makindo, hukindana na imani
   Ukabaki kando - kando, ukawa mbali na dini
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
7. Kitu kharabi mfundo, usiwe nao rohoni
   Usikae nao kondo, ukakerekwa moyoni
   Bwaga nafsi kwa pendo, usijiweke shindani
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
8. Jitanafasi matendo, mema si ya subiyani
   Acha mfundo si lindo, la kukuhami usoni
   Huo mkali uvundo, waleta karaha ndani
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
9. Alojawa na mfundo, hubanwa kitu kooni
   Huijenga chuki lundo, katika mtima chini
   Si mwenye kula uhondo, hatii chema kinywani
   Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
10. Siku zote kwake ngondo, nasaha kwake uduni
    Abaki kwenye utando, wa makosa ya huzuni
    Huzowa dhambi za shindo, ni nini hizo ni nini?
    Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
11. Usiwe nunda wa Mwendo, ni nani siye ni nani
    Kunjuwa nafsi nyundo, hushindiliwa mpini
    Sufu huliwa na nondo, hilo unalibaini
    Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
12. Jiwe si nazi si bondo, nazi huvunjwa chumani
    Huchujwa tuwi lingindo, hupikwa kikaangoni
    Likaungiwa mandondo, wewe wasema "katwani"
    Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
13. Lete nafsi lawwama, tusijirudi kwa nini?
    Leo aula mtondo, lifikirie makini
    Ngangari ina mtindo, hata ya sawa kuhini
    Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu
14. Ah! Ola makamando, wajuzi wa hii fani
    Wameelewa mfundo, unahusu kitu gani
    Hao watwaa mipondo, waja kutuvusha pwani
    Wenye mfundo Madobi, zifuweni nyoyo zenu

Al-Ustadhi Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu
S.L.P 376, Dar es salaam.

EWE MOLA TWAKUOMBA - UINUSURU JAMAAT

1. Mwenyezi Mungu Muumba, ardhi na samawati
   Na vilivyomo sambamba, vyake Amevidhibiti
   Vinene pamwe vyembamba, vyote vyapiga saluti
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
2. Ni sikitiko Muumba, nawakilisha kwa beti
   Naleta kwako naimba, Tusaidie bahati
   Watu wanatuperemba, kwa zana zenye ghalati
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
3. Allah, tulo kwenye Nyumba, ya Ahmad bayiti
   Usalama wetu samba, twatishwa kila wakati
   Wataka tufe masamba, tikitiki na fofoti
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
4. Wametuwekea chemba, kwa huko walikoketi
   Wanataka hii nyumba, kamwe tusikarabati
   Kwa chini wanaichimba, juu waezuwa bati
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
5. Kuna watu wamanamba, wa maumbo tofauti
   Hao Bwana wanatamba, dhamiri kutusaliti
   Madhumuni yako kwamba, ifutike Jamaati
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
6. Kila pande wanatamba, wanena kwenye buyuti
   Wameamuwa ya kwamba, Ahmadiyya wafute
   Wametayarisha kamba, tufungwe hadi mauti
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
7. Mambo sasa yamepamba, tunasakwa kama nyati
   Nia yao kututimba, watukanyage mafuti
   Akheri tufe kibomba, tusitowe hata khati
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
8. Hivi sasa makaramba, mchana na lailati
   Wameshaanza kugomba, kuturushia baruti
   Tuwapo kwenye kuomba, ndanimwe mwa misikiti
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
9. Mabomu wanajipamba, kama watu hasanati
   Wanavaa na vilemba, kwa makanzu na makoti
   Ni watu, lakini mamba, ni wakubwa wafiriti
   Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
10. Hao wakwega kasumba, bangi na mihadharati
    Mashavu yamewavimba, wangetambuwa laiti
    Nao wameziba pamba, hawasikii swauti
    Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
11. Wanabeba na kusomba, silaha za ainati
    Wanajifanya miamba, wabeba magirineti
    Waje wabomowe nyumba, ndanimwe siye twaketi
    Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
12. Ya Allah, Ewe Muumba, ni yupi tena Mufti?
    Ni Weye Mwamba wa myamba, jeuri kwako hapiti
    Humnasa bila kamba, wa ghorofa na makuti
    Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
13. Subhana twakuomba, kwa maduwa na swalati
    Kwa kwikwi zisizo namba, uinusuru Jamati
    Na hao wanaotamba, watambae kwa magoti
    Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba
14. Hila zao ziwe nyamba, zipukutike pukuti
    Ziyeyuke kana kwamba, pinde za mvua ya kati
    Jumuiyya iwe shamba, iwe kito cha yakuti
    Uinusuru Jamati, Ewe Mola twakuomba

Al-Ustadhi Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu
S.L.P 376 Dar es Salaam.

Barabara kuelekea Jumuiya Ahmadiyya

Na Mwalimu Rashid Mussa Ungando

Mara nilipomaliza mafunzo ya Ualimu kule T.T.C Mpwapwa mwaka 1943, kwa mara ya kwanza nilipelekwa kufundisha katika shule ya Msingi ya Muhoro. kwa nyakati hizo ilijulikana kama N. H. School Mohoro Wilayani Rufiji (Eastern Province).

Baada ya miezi michache nilipatwa na udhaifu wa afya ulionifanya nishindwe kufika darasani kwa muda wa mwezi hivi. Muda huo wote niliutumia nyumbani kwa kusoma vitabu kutoka maktaba ya shule. Kilinivutia kukisoma kitabu cha "Uhuru wa Watumwa" kilichoandikwa na James Mbotela na Tafsiri ya Qur'ani ya Kiarabu kama alivyoiandika Padre Godfrey Dale.

Kwanza nilianza kukisoma kitabu "Uhuru wa watumwa" humo niliona jinsi mwanadamu alivyotendewa kikatili sana na kuvuliwa utu wake wote. Na mwisho wa lawama zote zilizowapata watumwa ziliajibishwa katika dini Tukufu ya Kiislamu. Hivyo ikawa kila niliyemdhania kuwa Sheikh nilianza kumuuliza maswali kuhusu Uislamu na Biashara ya utumwa. Na kisha "Mtwana na Mjakazi". Wengi miongoni mwa Masheikh nilioweza kuwaswali, walipendelea kuwepo "Ubwana na Utwana katika Dini ya Kiislamu". Hivyo duku duku langu juu ya utumwa na mateso ya watumwa likabaki vivyo hivyo.

Baada ya hapo nikaendelea kuisoma Tafsiri ya Qur'an Tukufu. Tafsiri ya Padre Dale. Kama kawaida kwanza nilianza kuisoma Dibaji yake yote. Humo namo nikashuhudilia mambo mazito zaidi, na niliyoyaona kuwa ni mazito ni kama haya:-

(i) Katika dibaji yake Padre Dale alitamka kuwa "Nimeonywa na Mapadre wenzangu kwani kwa kufanya tafsiri hii ya Qur'an ya Kiarabu huenda ikasomwa na baadhi ya Wakristo ikasababisha baadhi yao kujitenga na Ukristo na kuamini katika Uislamu". "Ninasema mkristo atakayeacha imani ya Kikristo na kujiunga katika Uislamu, ni sawa na mtu anayebadili taa yake ya dhahabu kwa taa



Mwalim Rashid Mussa Ungando akiwa na mwanafunzi mwenzake mpendwa

ya kibatari".

(ii) Ndoa ya Mtume Mtukufu (saw) na bibi Zainab binti Jahshi, aliieleza kama ni ndoa ya mtu malaya ambaye hastahili kudai kuwa Nabii na mtu aliyetumwa na Mungu kama Muhammad alivyodai.

(iii) Dini ya Kiislamu haiwezi kudai kuwa ni dini inayotoka kwa Mungu, kwa vile inawagawanya wafuasi wake kati ya; Waungwana, Watwana na Wajakazi.

(iv) Waislamu wa kwanza walionyeshwa upanga ndipo waliposilimu kwa nguvu. Hapo Padre Dale naye akaongezea kuniweka hoi baada ya kitabu cha uhuru wa watumwa.

(v) Padre Dale akaongezea kusema, "Ukikutana na Muislamu yeyote muulize kama anaye kiongozi kama sisi Wakristo tulivyo. Muislamu akitaja Mecca, kwa sababu tu kila mwaka wanakusanyika pale kuhiji. Na akitaja Madina, kwa sababu ya huyo kiongozi wao Muhammad amezikwa Madina. Kwa hali yoyote Waislam hawana kiongozi".

Hapo kweli Padre Dale aliendelea kuniweka hoi. Mwaka 1952 nilihamishwa kutoka Wilaya ya Rufiji kwenda kufungua shule katika Wilaya ya Bagamoyo. Kwa vile kutoka Bagamoyo mjini mpaka kule nilikokwenda kufungua shule mpya ni umbali wa Km.170 hivi, nikafikiria kupata gazeti la kunichangamsha, nikaamua nipate gazeti linalotoka kila wiki kwa wakati huo ambalo lilikuwa gazeti la "Baraza" likitoka katika nchi ya Kenya. Katika gazeti hilo niliona tangazo la Qur'an Tukufu kwamba inatafsiriwa, na karibu itakuwa tayari.

Mfanyabiashara mmoja aliyekuwa karibu yangu na mzungumzaji wangu sana, alikwenda Morogoro. Alipopitia Morogoro Book Shop akaona kwa mara ya kwanza tafsiri mpya ya Qur'an Tukufu, akainunua kwa thamani ya Sh.20/= aliporudi nyumbani akanikabidhi mimi ile tafsiri. Kwa vile yeye mwenyewe bado anashughulikia biashara ya ununuzi wa nafaka. Niliipokea tafsiri na nikaendelea kuisoma. Mashaka yangu yote niliyoyapata katika kitabu "Uhuru wa Watumwa" na Tafsiri ya Qur'an ya kiarabu (Padre Dale) yakanitoweka.

Mwaka 1953 mwezi wa Disemba nilichukua likizo kwenda Mwanza kutokea Bagamoyo. Wakati nikirudi Mwanza kufika Station Tabora, nikakutana na muuzaji wa gazeti la Mapenzi ya Mungu, nikanunua nakala moja. Kwa mara nyingine tena nikaongezeka imani kwa Jumuiyya ya Ahmadiyya baada ya ile Tafsiri na sasa naona nyongeza nyingine ya gazeti la Kiislamu kama nilivyoliona.

Baada ya kurudi Bagamoyo nikajiona nimo katika orodha ya walimu wanaohama. Nilihamia katika shule ya Msingi ya Rusende Wilayani Rufiji. Pale shuleni Rusende ni umbali wa mita 500 mpaka "Nyipara kijiji alichofikia Sheikh Saleh Mbaruku kuleta ujumbe wa Seyyidna Ahmad (as) wilayani Rufiji.

Sheikh Saleh Mbaruku Kapilima aliwasili Nyipara / Rusende April 1954. Alipokelewa na wananchi wa kijiji cha Nyipara kwa busara yake alifaulu kusuhubiana na vijana waliopata kuhitimu Qurani kama vile kijana Juma Abdallah Mpitakunza na Rashidi Seif Njoka, ambao baadaye walijiunga katika Jamaat. Siku za kati Sheikh Saleh Mbaruku alifaulu kumkaribia sana Sheikh Mkuu wa Zone ya Rufiji ya chini (Lower Rufiji) Sheikh Mohamed Shamte Kironda kabla ya fitina kuja kuwagawa.

Vikaratasi vya mahubiri vilivyoletwa Nyipara kwa Sheikh Saleh Mbaruku alivitawanya kwa kuwatumia vijana niliowataja hapo juu, vilisaidia sana kuieneza Jamaat Ahmadiyya katika mzunguko wa kijiji cha Nyipara / Rusende. Mapema katika miaka ya 1955 / 56 ikawa tunatembelewa na Sheikh Abdulkarim Sharma na wengineo. Nilikata shauri na kujaza Baiat mwaka 1956. Pekepeke ndogo ndogo zilianza kujitokeza, na kati kati ya mwaka 1957 mjadala mkubwa ulifanyika hapo Rusende kwa wingi wa wananchi wasiopungua 3000 walihudhuria katika mjadala huo. Hawa ni watu wengi sana kwa wakati huo kabla ya vyama vya siasa kukusanya watu wengi sana kuzidi watu 3000 katika majadiliano upande wa Jamaat Ahmadiyya uliongozwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi na upande wa upinzani alikuwa Sheikh Masuud Khatibu Jongo.

Sheikh Masuud Khatibu Jongo alishindwa kujaribu kusoma aya au Hadithi yoyote mbele ya Sheikh Amri Abedi. Maneno ya sheikh Masuud Khatibu Jongo yalikuwa kama hivi - mimi nimesimama hapa mtoto wa Nyamketo kwa mama yangu, na kwa Baba yangu Jongo, hawa wote waliopo hapa wanahusika. Wewe je, anakujua nani hapa? Baadhi ya wachache wenye akili walichagua upande wa kuusikiliza.

Kwa vile mjadala huu ulikuwa chini ya udhamini wa Hakimu wa Mahakama ya mwanzo, ilimpasa Hakimu atoe uamuzi kuhusu "Ndoa". Sauti na ushauri wa Hakimu ulikuwa hivi, "Nimewaita hapa Masheikh wa pande zote mbili, nimewasikia. Sasa yule asiyeridhika na maelezo ya upande mmoja na anataka kuvunja ndoa lazima arudishe mahari na kutwaa binti yake".

Baada ya hapo Jamaat ikaendelea kijijini Nyipara mpaka mwaka 1974. Mwaka wa operation vijiji Jamaat ya Nyipara ikahamia kijiji kipya "Mkongo". Mimi sikuwahi kunyang'anywa wake, wake zangu wote wawili walijiunga katika Jamaat Ahmadiyya mpaka leo. Wananchi wa Rusende walitaka niondolewe katika shule ile, lakini D.C wa wakati huo Mr. John Young aliwajibu yeye ni Mkristo. Katika shughuli zangu kama D.C wa Wilaya hii sishughuliki na kuhubiri Ukristo. Na huyu Mwalimu wa shule kadhalika atashughulika na mafundisho aliyopangiwa na Wizara yake. Mkaguzi wa shule akifika katika shule hiyo akiona mafundisho ya dini katika daftari za watoto, ndio mwalimu huyo atakapoonekana kuwa anayo hatia. Lakini kuhamishwa kwa sababu ameamua kujiunga katika imani anayoitaka hakuna mtu wa kumuingilia kati.

Baada ya operation vijiji mwaka 1974 sehemu kubwa ya wanajumuiyya walitawanyika. Mimi nilipostaafu mwaka 1978 niliamua kukaa hapa kijijini, nilipo hivi sasa. Ikatokea baadhi ya Wanajumuiyya waliokaribu ya Kibiti walizidi kusogea na tukaungana kuanzisha tawi hapa, mwisho Makao Makuu ya Jamaat ya Rufiji yakastahili kuhamishiwa hapa Kibiti, ambapo hivi sasa pamejengwa Msikiti mkubwa na kustahili kuwa Makao Makuu ya Zone ya kusini ya Mkoa wa Pwani.

Mwandishi - Rashidi Mussa Ungando
Box 28 Kibiti.

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

KUMBUKUMBU YANGU

Chochote hakikuvuruga utulivu wake, imani yake ilikuwa imara kukikabili chochote, na ikamtetea katika hali zote.

Akakaa pamoja na Hadhrat Ummul Muminin kwa nusu saa ambamo msingi wa urafiki baina yao uliwekwa ambao ulidumu maisha yake yote. Tuliporejea nyumbani, alikuwa hana budi kufikiri kwamba katika kitambo cha masaa mawili hivi ataagizwa kuhudhuria kukabili jaribio gumu mno la maisha yake. Lakini alikuwa na yakini kwamba hatua aliyochukua aliagizwa na Mungu kuichukua hata kwamba hakuwa na shaka kwamba Yule Aliyemwongoza mpaka sasa Atamsaidia daima dawamu. Hakuhitilafiana na mumewe hapo kabla katika jambo lolote kubwa, lakini sasa wakakabili jambo zito lihusulo wokovu wa roho zao. Akisubiri kurudi kwake nyumbani haikosi akaomba sana mwongozo na nguvu.

Akawasili, na tena nikabahatika kupata nafasi ya kusuhudia yaliyotokea. "Je, ulikwenda?" Akauliza kwa hamu na shauku, akiongeza sawa na kawaida yake maneno ya kuonyesha upendo.

"Ndiyo, nilikwenda."

"Tena?"

"Mtu huyo ndiye"; akitetema kidogo.

"Natumaini hujafanya uamuzi wa mwisho."

Akaweka mkono wake wa kuume juu ya moyo wake na akahakikisha: "Nimefanya baiati."

Uso wake ukafifia rangi, na midomo yake ikamtetemeka, lakini akajaribu sana kujizuia na akanung'unika: «Haikutendeka vizuri."

Kisha akamwita mtumishi na kumwamuru:

"Ondoa kitanda changu ukipeleke katika chumba cha pili."

Hapo mama akapaza sauti kidogo na kumwambia mtumishi: "Peleka kitanda chake katika makazi ya wanaume!"

Hiyo haina budi ikamshangaza, kwani akasema kwa uchungu: "Kwa nini?"

"Kwa sababu Mungu kwa hisani Yake Amenijaalia kuona mwanga, nawe bado umo gizani!"

Akatambua kwamba mama kashinda. Akamgeukia mtumishi na kumwambia aondoke hapo akisema kwa masikitiko: "Mama hana budi kushinda."

Kipeo cha hatari kikapita, kila mmoja akatulia; lakini baba yangu bado akatakiwa kuamua; mama yangu akafululiza kufanya maombi kwa mwungano wao kiroho.

Mwanasheria mmoja mwenzake kule mahakamani pia alikuwa na moyo wa kuipenda Jumuiya; baba yangu aliyeelekea mwenyewe kusonga mbele akamwuliza kama atashirikiana naye. Mwenzake akapenda kupata maelezo bayana kuhusu baadhi ya mambo fulani makubwa, na ikakubaliwa wapate mwongozo kutoka kwa Maulawii Nuruddin r.a. ambaye kwa ukarimu akawaarifu kwamba atafurahi kuonana nao kila jioni kwa muda wa saa moja hivi. Katika vikao vinne mimi pia nilipata bahati njema kuhudhuria. Hiyo ikanipa nafasi ya kumwangalia Maulawii Nuruddin r.a. kwa karibu sana; yeye naye pengine akaniangalia kama mwana wa rafikiye Nasrullah Khan. Akirudi kutoka kikao cha mwisho, baba yangu akamwuliza mwenzake kama yeye anaweza sasa kufanya uamuzi. Akasema, maswala aliyouliza yametatuliwa yote.

Baba yangu akauliza: Je, basi, tutafanya baiati?"

"Wafikirije?" Akauliza.

"Niko tayari, kama uko"

"Vizuri sana, basi. Kesho asubuhi ukija kwenye sala ya Alfajiri, nichukue pia pamoja nawe, nasi tutafanya baiati."

Kesho asubuhi nikafuatana na baba yangu kwenda kusali sala ya Alfajiri pamoja na jamaa; njiani kwenda msikitini tukamtaka mwenzake kufuatana nasi, lakini akaona bado hayuko tayari kubeba jukumu lilazimishwalo na ahadi ya baiati. Basi babangu akafanya baiati faraghani akikaa na Masihi Aliyeahidiwa baada ya sala ya Alfajiri. Nilikuwapo pia. Kufanya baiati kwa babangu muda kidogo baada ya baiati ya mamangu ilikuwa pia sawa na ruya mojawapo ya mama. Mapatano yakarudishwa kwa furaha katika familia. Miaka kumi baadaye ukatokea msukosuko, lakini mambo yakarekebishwa kwa njia hiyo hiyo.

Baada ya kujiunga katika Jumuiya, baba yangu akakaa Qadian siku nyingi zaidi za Septemba, mwezi wa likizo ya korti za wilaya. Akahudhuria pia katika kila Mkutano wa Mwaka uliofanywa katika wiki ya mwisho ya Disemba. Nikafuatana naye kila mara. Huko kulikuwa na fursa ya kuwa pamoja na Masihi Aliyeahidwa alipokwenda kupunga hewa asubuhi na alipokaa katika msikiti (Masjid Mubarak) baada ya sala ya Adhuhuri, na baada ya sala ya Alasiri. Muda uliobakia nikafaidika na kila nafasi niliyopata kukaa na



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. Nakumbuka kwamba kwa muda fulani alikuwa akisomesha kabla ya saa sita za mchana *Mathnawi* ya Maulana Jalaluddin Rumi.

Baada ya kumaliza darasa la kumi mnamo Aprili 1907, nikaingia Government College Lahore kwa kozi ya Shahada ya Chuo cha Panjab mnamo Mei. Katika likizo za kiangazi za mwaka huo nilipokuwa nyumbani baba yangu akapokea kadi ya posta (barua) kutoka kwa Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. iliyomaanisha nifanye baiati ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Nilivyoona mimi, nilikuwa mwanajuwuyia wa Kiahmadiyya tangu Septemba 3, 1904, nilipopata bahati kuuona uso uliobarikiwa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. mjini Lahore, na nikajihesabu nimo katika baiati za wazazi wangu walizofanya wiki chache baadaye mjini Sialkot nami nilikuwapo hapo. Hata hivyo kwa kufuata agizo la Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. lililotolewa kwa baba yangu, nikafanya baiati kwa mkono wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika Qadian tarehe 16 Septemba 1907. Namshukuru sana mno Hadhrat Maulawii Sahib r.a. kwa kutoa agizo lake hilo, kwani alipofariki Masihi Aliyeahidiwa tarehe 26 Mei 1908, orodha tukufu ya heshima ya masahaba zake ilikamilika na kufungwa. Siku hiyo ya msiba mkubwa kabisa na huzuni ya kushinda nilikuwa Lahore na nikafuatana na mwili wa kiongozi aliyeaga dunia, hadi Qadian ambako keshoye jioni Hadhrat Maulawii Nuruddin alitangazwa kuwa Khalifatul Masihi, na wanajumuiya wote wa Kiahmadiyya waliokuwako Qadian, nikiwa mmojawapo, wakafanya baiati kwake.

Katika muda niliokuwa katika College (chuo) niliendelea kutembelea Qadian mara kwa mara, nikakaa huko sehemu ya likizo za kiangazi na kuhudhuria Mkutano wa Mwaka kama kawaida kila mara. Hivyo nikajulikana kwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. na nikapokea hisani zake nyingi kwa ukarimu wake na misaada kutoka kwake.

Baada ya mtihani wangu wa mwisho wa kupata shahada mnamo Arpili 1911, nilikwenda kwetu Sialkot na baada ya kukaa huko kwa wiki kadhaa nikaenda Qadian mnamo mwezi wa Juni. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa bado mgonjwa, akipitisha mchana katika sebule akitoa darasa, kushughulikia kazi za Jumuiya, kuwaangalia wagonjwa na kupokea wageni. Jeraha la panja la kuume likawa donda la kudumu na likafungwa dawa kila siku. Baada ya kutembelewa na daktari akaendelea kulala kwa kitambo, na mwanafunzi wake mmojawapo akamkanda mikono na miguu taratibu. Alikuwa bado hajapata nguvu ya kwenda msikitini kwa sala za kila siku hivyo zilisaliwa katika sebule yake kwa ajili yake. Mwanafunzi wake aliyempenda na aliyekuwa anamsimamia, Sheikh Muhammad Taimur, aliongoza sala; Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akasali akikaa. Maamuma walikuwa wanafunzi wanne au watano. Iliposikika adhana kutoka msikiti wa karibu zaidi Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akamwagiza kila mmoja aondoke akaungane na sala ya jamaa msikitini. Siku ya kwanza ya ziara yangu, adhana ya sala ya adhuhuri iliposikika na wote waliambiwa kwenda nikainuka kuondoka. Ndipo Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kwa ukarimu na upendo akaniagiza: Mian, utasali hapa pamoja nasi. Hivyo, nikasali sala ya adhuhuri pamoja na jamaa katika sebule.

Kulikuwa na mstari mmoja tu wa waabuduo nyuma ya Imam. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akakaa upande wa kushoto kabisa baada ya kitanda chake. Nikasimama upande wake wa kuume na maamuma wengine wakajipanga kulia kwangu. Kwa sababu ya kupenda nisimsumbue na pia kwa kumheshimu sikusimama karibu sana naye, lakini akaweka mkono wake kuzunguka miundi yangu na akanisogeza karibu yake. Safari moja ambapo Sheikh Muhammad Taimur hukuwepo hapo kuongoza katika sala ya alasiri, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaangalia huko na huko, akaniambia: Mian, umekwisha soma Qur'an Tukufu, tafadhali uongoze katika sala. Nikalazimika kutii.

Siku moja ikawa hivi kwamba daktari alipoondoka baada ya kumfunga dawa jeraha lake, nilikuwa peke yangu ndani ya chumba. Sikujua kukanda sawasawa. Je, niondoke chumbani taratibu, ama nijaribu kumkanda mikono na miguu mgonjwa mheshimiwa – jambo litakalomsumbua pengine kuliko kumpa raha? Ilivyokuwa desturi yake, akalala kwa ubavu wake wa kushoto. Nikaenda taratibu kukaa juu ya kitanda chake nyuma yake, nikaanza kutoa utumishi wangu kwa hadhari na kushikashika kwa vidole vizito. Baada ya dakika tano hivi nikaacha, kwa nia ya kuondoka na kumwacha apumzike. Alipotambua hiyo, akainua mkono wake wa kuume na akauweka pembezoni mwa shingo yangu, akauelekeza uso wangu kwa upole karibu na uso wake, akaniweka katika hali hiyo kwa dakika mbili hivi akiwa kimya. Aliponiacha, akanena: "Mian, nimekuombea maombi mengi sana!" Kweli, ilikuwa dua ya heri ambayo harufu yake njema imedumu nami miaka sabini.

Nilipokuwa bado Qadian babangu akaniandikia nimpelekee Hadhrat Khalifatul Masihi maombi kadha wa kadha, mojawapo katika hayo lilikuwa kumwomba ruhusa kwamba niende Uingereza kwa masomo ya juu. Nikampelekea maombi hayo katika maandishi. Kunihusu mimi nikaandika kwamba, kwa fadhili ya Mungu, nimefanya vizuri katika mtihani wangu wa Shahada ya B.A. na kwamba natumai nitapita, na kama akitoa kibali na kuniruhusu, baba yangu anapenda niende Uingereza kwa masomo ya juu. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaagiza ya kwamba baba yangu na mimi twapaswa kutafuta mwongozo wa Mungu kwa sala ya *Istikhara* kwa njia iliyofundishwa. Na kama sote wawili tukiridhika baada ya sala hiyo, nitaweza kwenda kama alivyotaka baba yangu. Nikamwarifu baba yangu agizo lake na nikaomba mwongozo wa Mungu kwa wiki moja, hatimaye nikahisi dalili dhahiri kuafikiana na upendo wa baba yangu, ingawaje binafsi sikupenda kwenda ng'ambo.

Matokeo ya mtihani yalitangazwa, na rafiki mmoja kutoka Lahore akaniandikia kwamba nimepita katika Divisheni ya Kwanza. Nikampelekea barua hiyo Khalifatul Masihi r.a. ambaye alifurahi sana hata kwamba kila mmoja aliyemjia kumwona jioni hiyo akamwambia: "Nina furaha kubwa leo, huyu, akiashiria kwangu, amefaulu katika mtihani wake wa B.A., tena ni la ajabu kwamba alijua atafaulu."

Ikajulikana baadaye kwamba nilikuwa wa kwanza katika Arabic Honours (Daraja la juu la Kiarabu). Na kama ningelikuwa na nia ya kufanya M.A. kwa Kiarabu, ningelipatiwa malipo ya kutosha kwa kuendelea na masomo hayo.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Islam sio Dini ya vurugu, bali ni Dini ya amani, subira na maelewano

Na Mwl. Kaisi Ali -
Mkongotema, Songea
(0714920017)

Mwenyezi Mungu Amesema katika Qur'an Tukufu kwamba;
"Wala msifanye uharibifu (fujo) katika nchi ikisha tulia, na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumaini. Bila shaka rehema za Mwenyezi Mungu zi karibu na wafanyao hisani" (Qur'an 7:57)

Tena Anasema Mwenyezi Mungu;
"Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama mwapavyo) ndugu, na Anakataza upujufu, uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu" (Qur'an 16:91).

Tena Anasema Mwenyezi Mungu;
"Na Mwenyezi Mungu hapendi uharibifu" (Qur'an 2:206).
Ndugu zangu wapendwa aya hizo nilizozinukuu hapo juu kutoka katika Qur'an Tukufu zinaeleza kwa uwazi kabisa kwamba Mwenyezi Mungu Amekataza kufanya fujo hapa duniani. Hivi karibuni Mwezi wa Octoba, 2012 sawa na taarifa zilizoripotiwa kutoka katika vyombo vya habari vilieleza kwamba baadhi ya watu wanaojiita kuwa Waislam wa jijini Dar es salaam, walifanya maandamano yaliyosababisha kuvunjika kwa amani na kupelekea kuchomwa kwa majumba ya ibada yaani Makanisa. Na baadhi ya watu walipoteza mali zao kwa kuibiwa na watu wasiojulikana, pia na wengine waliumizwa kutokana na vurugu hizo, kupelekea Jeshi la Polisi kufanya kazi yake ya kutuliza ghasia kwa kuwakamata watu hao waliotuhumiwa kuanya fujo hizo.
Ndugu wasomaji wapendwa kwanza napenda kutoa pole nyingi sana kwa wale wote walioathirika kutokana na mkasa huo hasa kwa ndugu wapendwa Wakristo ambao hasa ndio wahanga waliochomewa Kanisa lao ambalo ni nyumba ya ibada, na pia ninatoa masikitiko makubwa kwa wale waliofanya matendo yale ya kihuni ya kuchoma moto Kanisa, na kuharibu mali za watu. Hivyo basi napenda kuuleza uma wa dini zote kwamba matendo hayo maovu yaliyofanywa na hao watu wanaojiita ni wafuasi wa dini tukufu ya Kiislam hayaungwi mkono kabisa na mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam.
Hivi karibuni tarehe 05/11/2012 nikikwa Songea Mjini katika maeneo ya soko kuu la Mkoa wa Ruvuma nilikutana na Rafiki yangu ambaye ni Mwislam Msuni Bw. Hakimu ambaye ni mfanya biashara wa samaki katika soko kuu la mkoa aliniuliza maswali yafuatayo kwamba Je, una maoni gani kuhusiana na Sheikh Isa Ponda aliyewekwa ndani rumande na Serikali? Na Je, una maoni gani na wale ndugu zetu Waislamu waliochoma moto Makanisa? Nilimjibu kama ifuatavyo, kuhusu Sheikh Isa Ponda Serikali ndio inajua zaidi, kuhusu habari zake Serikali bado inaendelea na uchunguzi na kama ikibainika hana kosa lolote basi Serikali itamwachia huru, na kama ikibainika anayo makosa basi sheria itachukua mkondo wake.

Na kuhusiana na wale waliochoma moto Kanisa kama ni waislam, basi wamefanya makosa makubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu, nikaendelea kumweleza kwa kumsomea aya za Qur'an Tukufu zisemazo kwamba;
"Imeruhusiwa (Kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa, na kwa yakini Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuwasaidia, waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema Mola wetu ni Mwenyezi Mungu na kama Mwenyezi Mungu Asingeliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa, Mahekalu, na Makanisa na nyumba za ibada na Misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu Hutajwa kwa wingi, na bila shaka Mwenyezi Mungu Humsaidia yule anayemsaidia yeye, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mshindi" (22:40 - 41).
Baada ya kumsomea aya hizo hapo juu nikamweleza kwamba kwa mujibu wa aya hizo hapo juu Mwenyezi Mungu Anawaeleza Waislam kwamba wawe tayari na hata ikibidi wakubali kufa kuyalinda majumba ya ibada yakiwemo pamoja na Makanisa. Kufika hapo Bw. Hakimu alishikwa na butwaa na akaanza kuniuliza maswali mara tatu tatu akisema kwamba hivi ni kweli aya hizo zipo ndani ya Qur'an Tukufu?! Kisha akazinukuu aya zile na akasema kwamba anaenda kuziangalia zaidi ndani ya Qur'an Tukufu kwa sababu alisema 'toka nizaliwe sasa hivi nina umri wa miaka 55 lakini aya hizo sijawahi kuziona wala kuzisikia', akaendelea kusema kwamba 'leo hii ninaona kama aya hizo ndio kwanza zinashuka kutoka kwa Mwenyezi Mungu', na akasema kwamba 'nikiziona aya hizo basi nitawaonyesha na wenzangu pia, halafu nitakupigia simu ili kukueleza'.
Tarehe 13/11/2012 Bw. Hakimu alinipigia simu na kunieleza kwamba ni kweli zile aya zipo ndani ya Qur'an Tukufu na zinaeleza kama ulivyonieleza kwamba Waislamu wameambiwa na Mwenyezi Mungu kwamba wayalinde majumba ya ibada yakiwemo na Makanisa. Bw. Hakimu akamalizia maelezo yake kwa kunitania akisema kwamba Ahmadiyya wameshinda kwa hoja.

Zama za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ili kuonesha kwamba Mtume Muhammad



Mwl. Kais Ali

(saw) alikuwa na mahusiano mazuri na watu wa dini zingine, safari fulani ujumbe mmoja wa Wakristo kutoka katika eneo la Najran ulifika mjini Madina kwa ajili ya kufanya mjadala wa mada za tofauti baina ya Islam na Ukristo, walikaa Madina siku tatu. Ulipofika muda wao wa kusali walianza kujadiliana ndani ya ule msikiti wa Mtume (saw) kutafuta mahali pa kusalia, walimwomba ruhusa Mtume Muhammad (saw) ili watoke nje kwa minajili ya kusali sala yao. Mtume (saw) aliwaambia kwamba msikiti pia ni mahali pa ibada, wanakaribishwa kusali mule msikitini. Ndipo wale Wakristo wakasali ndani ya Msikiti ule wa Madina wa Mtume Muhammad (saw) muda si mrefu wakafika mule msikitini baadhi ya Masahaba na wakawaona wale Wakristo wakisali wakielekea Mashariki, tofauti kabisa na wanakoelekea Waislam wakati wa sala zao, wale Masahaba wakasogea mbele ya Mtume (saw) ili kutaka kupinga jambo lile la Wakristo kufanya ibada mule Msikitini. Lakini Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwa moyo wa uthabiti akawakataza Masahaba wasiwabughudhi wale Wakristo na Mtume (saw) akatamka akasema;
"Mimi nimewaruhusu kwa sababu hii ni nyumba ya Mungu, na hakuna mwenye haki ya kumkataza yeyote yule mwenye kumwabudu Mungu katika mahali palipo wakfu kwa minajili ya ibada".
Pia safari nyingine ulitumwa ujumbe kutoka makao makuu ya watawa wa kikristo ya St. Catherine kwenda kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) waliandika tangazo lililosema kwamba makao makuu yao yapatiwe ulinzi wakati Islam itakapopata ushindi katika sehemu zile za dunia, Mtukufu Mtume Muhammad (saw) mara moja akalikubali ombi lao lile na akaandika amri za kutekeleza, akisema kwamba;
"Haimpasi mtu yeyote kuingilia rasilimali za makao makuu ya watawa, wala sanamu ya msalaba au kitu chochote kinachowakilisha dini yao, na visiharibiwe kwa njia yoyote iwayo. Yeyote atakayelipuuza jambo hili hatakuwa mmoja wetu".
Amri hizi zipo zimehifadhiwa katika nchi ya Uturuki. Hivyo basi napenda kuwaeleza ndugu zangu wapendwa wa dini zote hasa ndugu zangu Wakristo kwamba, dini tukufu ya Islam ni dini ya amani, unyenyekevu na maelewano na watu wa dini zingine. Kama mlivyoona maelezo ya hapo juu namna Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alivyowafanyia wema watu wa dini nyingine. Hivyo basi vurugu zote na fujo zinazofanywa hapa duniani na baadhi ya vikundi vinavyojiita vya Kiislam hazina baraka na wala havina uhusiano wowote na mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam. Bali wao wanafanya vurugu na fujo kwa kutafuta maslahi yao. Pia zama za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) safari moja Bedui mmoja asiyekuwa Mwislam alikuja kutembea Madina na akakaribishwa kulala Msikitini. Lakini mtu huyo kwa kutojua, alianza kujisaidia haja ndogo mule mule Msikitini ambapo ni sehemu takatifu ya kufanyia ibada, na haja hii ndogo alijisaidia wakati Mtukufu Mtume Muhammad (saw) yupo mule mule Msikitini pamoja na Masahaba zake. Baadhi ya Masahaba zake walikasirishwa sana na kitendo kile hata wakatamani kumcharaza bakora yule Bedui lakini wakakatazwa mara moja kufanya hivyo, na Mtume (saw) akawaambia wamwache wasimbughudhi wakati anapojisaidia. Yule Bedui alipomaliza haja yake, Mtume (saw) aliitisha ndoo ya maji na yeye mwenyewe Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alipasafisha mahali pale. Kisha akawageukia Masahaba zake na akawaambia;
"Nyinyi hamkuinuliwa na Mungu kuwapatia watu shida. Daima kumbukeni ya kwamba mliinuliwa kuwaletea wanadamu faraja".
Ndugu wasomaji wapendwa kuhusiana na maelezo hayo ya hapo juu pia mmekwisha jionea wenyewe kwamba, ni jinsi gani Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alivyokuwa mtu mwenye upendo, huruma na maelewano na watu wa dini zingine. Hivyo basi narudia tena kusema vurugu zote na fujo zinazofanywa na baadhi ya makundi yanayojiita ya Kiislamu hapa duniani hayana uhusiano wowote na mafundisho ya dini tukufu ya Kiislamu bali wao wanatafuta maslahi yao ya dunia na kutafuta vyeo. Pengine vurugu hizi zinazofanywa na baadhi ya vikundi vinavyojiita vya Kiislam, wanafanya hivyo eti wakieleza kwamba wao wanafanya jihadi yaani wanapigana vita na makafiri wa dini ya Kiislam.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Apata 'chamtemakuni'

Kutoka uk. 12

hivyo mara akatokea kijana mmoja ajulikanaye kama Al-ustadhi Issa bin Issa mara moja akamrukia Sheikh na kumkamata kwa nguvu na kumtikisa vya kutosha mithili ya mwizi, kisha akamuuliza naomba unijibu kuwa ni nani aliyekuruhusu uswalie jeneza hili? Je hujui kuwa huyu ni Ahmadiyya? Je uliwahi kuongea naye wakati wa uhai wake juu ya imani uliyokuwa nayo naye akakukubalia kuwa kauacha U-Ahmadiyya wake? Je unataka kumsilimisha maiti? Unataka kutuletea aibu gani hapa kijijini kwa upuuzi wako?!
Ndipo hata wafuasi wake wakajiweka pembeni na kumwambia kama anataka kuzika basi afanye mwenye mambo yote hadi mwisho. Masikini Sheikh Hamza alidhalilika sana, na mwisho alijikaza kisabu kuja kutuomba msamaha ya kwamba tuusitiri mwili wa ndugu yetu kwani walikuwa wamefanya makosa na hivyo kusababisha kuudhalilisha mwili wa marehemu.

Hapo tuliwasiliana na uongozi wa Jamaat Mkoa, na tukapata idhini ya kuusalia mwili huo na kwenda kuuzika. Baadaye nikapata fursa ya kutoa darsa na hapo nikatumia fursa hiyo kueleza mambo ya msingi yanayotakiwa katika mazishi na kupambanua baadhi ya bidaa zinazoongezwa na Masheikh wa siku hizi. Watu walionekana kufurahia na kusikika wakisema 'jamani tusome'.

Kwa upande wake Sheikh Hamza hali iliendelea kuwa ya aibu zaidi kwake, kwani Sheikh mkuu wa Msikiti pale kijijini alitoa hotuba kali na kusema kuwa "Makadiyani sio Waislam, kwa hiyo Mwislamu yoyote hatakiwi kusimama na kusaliya jeneza la kafiri, na kwamba aliyefanya hivyo amefanya kosa kubwa sana na hivyo hatakiwi kushirikiana nasi hapa msikitini kwetu".

Ingawa hotuba hiyo ya Sheikh inaonyesha dhuluma ya hali ya juu kutuita Ahmadiyya kuwa ni makafiri na sio waislam, kwani Mtume (saw) alikataza kumuita kafiri mtu yeyote anayejiita Muislam. Lakini pia inafaa wale Masheikh kama akina Hamza wakumbuke kuwa haitawasaidia kugombea miili ya marehemu ambao wakati wa uhai wao waliwaita makafiri kisha wakishafariki wanataka kuwasilimisha. Hili ni kosa kubwa na inafaa wajifunze na kuepuka mwenendo huo, kama ambavyo wameona Bwana Hamza alivyofedheheka na kupata chamtemakuni.

Filamu inayokashifu Islam yalaaniwa

Kutoka uk. 11

1.8 ya Waislamu wanaonesha upingaji wao kama watoto'. Ikiwa hakuna kiongozi basi watu wanatembea tu hapa na pale na upingaji pia huwa wa kitoto. Hivyo walikejeli lakini wakadhihirisha ukweli pia. Mwenyezi Mungu Ajaalie kuwa Waislamu sasa waone soni.

Watu hawa ambao jicho lao la kidini limepofuka, wasiojua kamwe daraja la ubora wa manabii, wanaonyamaza kimya hata baada ya kumvunjia heshima Hadhrat Isa a.s., watazichukulia hisia za Waislamu zinazooneshwa kwa ajili ya Mtume s.a.w. kama upingaji wa kitoto tu. Lakini kama nilivyosema kuwa katika mwaka 2006 nilielekeza juu ya jambo hili kuwa pangeni mpango madhubuti kiasi hiki kwamba mtu yeyote asidiriki tena kufanya upuuzi wa aina hii. Laiti nchi za Kiislamu zingesikia hili na kila Mwahmadiyya awezaye kuwafikia basi ajitahidi kuwafikishia hili kwamba: Kufanya maandamano kwa siku chache na kunyamaza, hakutatatua suala hili. Vilevile kuna pendekezo lililopendekezwa kama ilivyo kawaida kwa watu kutoa mawazo, kwamba mawakili Waislamu wa dunia nzima wapeleke maombi ya malalamiko kwa pamoja. Laiti mawakili Waislamu wenye hadhi ya kimataifa wafikiri juu ya hayo, watafakari juu ya uwezekano wa jambo hili au watafute njia nyingine. Mpaka lini mtaendelea kutazama upuuzi wa aina hii ukifanyika na mtakaa kimya baada ya kufanya maandamano na kuharibu mali na majengo katika nchi zenu. Haya yote hayataiathiri dunia hii ya kimagharibi hata kidogo wala hayatawaathiri wale waliotengeneza filamu hii. Kama katika nchi hizi mtawashambulia watu wasio na hatia au mtawatishia au mtajaribu kuwaua au mtazishambulia balozi, basi haya yote ni kinyume na mafundisho ya Kiislamu. Islamu hairuhusu asilani kufanya hivyo. Kwa matendo hayo wenyewe mtatoa nafasi za kumsingizia Mtume s.a.w. Hivyo basi mabavu sio jibu lake. Jibu lake ni lile nililokwisha sema kuwa mrekebishe matendo yenu na kumwombea rehema na amani yule Nabii s.a.w. ambaye ni mwokozi wa binadamu wote. Na kwa ajili ya jitihada za kidunia nchi za Kiislamu ziungane pamoja, Waislamu waishio katika nchi za kimagharibi wathibitishe nguvu ya kura zao. Wanajumuiyya popote pale walipo, wafuate njia hii na vilevile wajitahidi ili marafiki zao wasio Waahmadiyya wakanyage njia hii hii kwamba: thibitisheni nguvu yenu na nguvu ya kura zenu katika nchi hizi. Ifahamisheni dunia, tabia njema za maisha ya Mtume s.a.w. kwa namna nzuri. Hivi leo watu hawa wanaopiga kelele ya uhuru wa kuongea, wanapiga kelele kwamba katika Uislamu hakuna hiyari ya kusema na uhuru wa kutoa mawazo na wanatoa mifano ya dunia ya Kiislamu ya siku hizi kuwa katika nchi za Kiislamu, wananchi na watu hawana uhuru wowote. Kama hakuna uhuru basi ni bahati mbaya ya nchi hizo kwamba hazifuati mafundisho ya Kiislamu. Uislamu haufundishi hivyo. Sisi twayakuta katika historia matukio yasiyo na kifani duniani ya watu kuongea na Mtume s.a.w. bila hofu yoyote - bali kwa utovu wa adabu - na juu ya hayo Mtume s.a.w. alionesha subira na uvumilivu. Naweka mbele yenu mifano michache tu, na ingawaje matukio haya yanaelezwa katika matendo ya ukarimu wa Mtume s.a.w. lakini matukio haya pia yanathibitisha kiwango cha juu cha kutomwogopa Mtume s.a.w. na uvumilivu wake.

Hadhrat Jubair bin Mutam r.a. anasimulia kwamba safari moja alikuwa pamoja na Mtume s.a.w. na watu wengine wakati wa kurejea kutoka Hunaini, mabedui walimng'ang'ania sana wakimwomba msaada hata wakamlazimisha kuegemea kwenye mti mmoja ambao miba yake ilinasa shuka yake. Mtume s.a.w. akasimama na kusema: "Nirudishieni shuka yangu na kama ningekuwa na ngamia sawa na idadi ya miti hii ya porini, ningewagawieni wala msingenikuta bahili wala mwongo wala mwoga. (*Sahih Bukhari kitabu Farzul Khumse babu ma kananabiyyu yutii ilmwullafate kulubehim wa gaerehim, 3148*).

Kisha kuna riwaya ya Hazrat Anas r.a., yeye anasimulia kwamba nilikuwa pamoja na Mtume s.a.w. naye alikuwa amejitanda shuka moja nene, bedui mmoja aliivuta shuka hiyo kwa nguvu kiasi hiki kwamba iliacha alama juu ya shingo ya Mtume s.a.w. kisha akasema: Ee Muhammad s.a.w., pakia sehemu juu ya ngamia wangu hawa wawili katika ile mali uliyopewa na Mwenyezi Mungu kwani hutanipa katika mali yako wala katika mali ya baba yako. Kwanza Mtume s.a.w. alikaa kimya kisha akasema "*almalu malullahu wa ana abduhu"* yaani mali ni Yake Mwenyezi Mungu na mimi ni mtumishi wake, halafu akasema maumivu uliyonipatia, utalipa fidia yake? Yule bedui akajibu: Hapana. Mtume s.a.w. akamwuliza: Kwa nini hutalipa fidia? Bedui akaeleza: Kwa sababu wewe hulipi ubaya kwa ubaya. Hapo Mtume s.a.w. akatabasamu na kuagiza kwamba pakieni shairi juu ya ngamia mmoja na tende juu ya ngamia wake wa pili. (*Alshifaa liqaadhi ayyaz juz awwal uku 74.....)*

Basi hiki ndicho kiwango cha subira na uvumilivu wa Mtume s.a.w. ambacho kilikuwa kwa maadui zake na jamaa zake. Hizo ndizo zile khulka za hali ya juu zinazoonesha ukarimu, subira, uvumilivu na ushupavu. Wapinzani hawa wajinga wanasimama na kumsingizia bila elimu yoyote yule aliye Rehema kwa walimwengu wote kwamba alitumia mabavu na akafanya hivi na vile.

Kisha nimesikia kwamba kuna upinzani juu ya Qurani Tukufu uliozushwa katika filamu hii. Mimi sijaitazama filamu hiyo lakini nimeelezwa kwamba ndani yake kuna madai eti Qurani tukufu hii iliandikwa na Warqa bin Naufal aliyekuwa binamu wa Bi Khadija r.a. ambaye Bi Khadija r.a. alimpeleka Mtume s.a.w. kwake baada ya kupata wahyi wa kwanza. Makafiri waliendelea kuleta upinzani huu hata katika zama za uhai wake kuwa Qurani hii unayoteremshiwa kidogo kidogo, kwa nini haiteremki mara moja ikiwa kweli ni neno la Mwenyezi Mungu? Lakini hawa watu hawanayo elimu hata kidogo bali hawaijui histotia pia. Kwa vyovyote vile, hiyo ni hali ya watengenezaji wa filamu hii lakini Mapadri wawili walio pamoja nao na wanajihesabu wenye elimu, nao ni wajinga wasio na elimu. Warqa bin Naufal alisema hivi: "Laiti ningekuwa hai wakati watu wako watakapokufukuza nchini" na baada ya muda mfupi akafariki. Hawa Mapadri, kama nilivyosema, hawajui kabisa historia wala hakika. Wachunguzi wa mambo ya mashariki daima walijadiliana kuhusu Qurani kwamba sura hii iliteremshwa wapi na sura ile iliteremshwa wapi, ilishuka Makka au Madina? Wanajadiliana juu ya jambo hili na kisha wanasema kwamba hii (Qurani) iliandikwa na yule (Warqa bin Naufal). Lakini hawaelewi kwamba Qurani yenyewe inatoa tambio kuwa kama mnaamini kuwa Qurani imetungwa na mtu basi leteni sura moja iliyo mfano wa hiyo (Qurani).

Kisha kuhusiana na kuziheshimu hisia za kidini, hata katika jambo hili Mtume s.a.w. hana mfano wake. Pamoja na kujua kwamba yeye ni mbora wa manabii wote, kwa kuzijali tu hisia za Myahudi alisema: "Msinipe ubora juu ya Musa."(*Sahih Bukhari hadithi no 2411).*

Juu ya kuzijali hali za mafukara, aliwapa heshima kwa namna hii kwamba safari moja, sahaba wake mmoja tajiri alikuwa anaonesha ubora wake wa mapato juu ya watu wengine. Mtume s.a.w. baada ya kumsikia alisema je umepata mwenyewe nguvu hii, uwezo huu na mali hii kwa mikono yako? La hasha, nguvu yako ya mali na ya watu zinatokana na mafukara. (*Sahihi Bukhari hadithi no. 2896*).

Wadai hawa wa uhuru, hivi leo wanadai kusimamia haki za maskini na kujitahidi kuzilinda na kuzitangaza pia lakini miaka elfu moja mia nne iliyopita kabla ya leo

Mtume s.a.w. alisimamia haki hizi kwa kusema: "Mwajiriwa apewe ujira wake kabla halijakauka jasho lake. (*Sunan ibne Majah hadithi no 2443*).

Basi hao watawezaje kushindana na yule Mbora wa wanadamu.

Kuna matukio chungu nzima na mkichukua khulka yoyote, mifano ya hali ya juu ya hiyo khulka itaonekana katika dhati ya Mtume s.a.w.

Kisha wameleta upinzani huu kwamba eti alikuwa na mapenzi sana na wanawake (Mungu apishe mbali na hayo) na wakaibua upinzani juu ya ndoa zake ambazo Mwenyezi Mungu aliukatalia mbali upinzani wao huu. Mwenyezi Mungu alijua kuwa matukio ya namna hii yatatokea na masuali ya aina hii yataibuka, kwa hiyo Alikuwa Akileta mazingira yanayokanusha hoja kama hizi. Inaelezwa kuhusu Asmaa bint Numaan bin Abi Jaun kwamba alikuwa miongoni mwa warembo wa Arabuni na yeye alipofika Madina, wanawake walienda kumtazama na kumsifu kwamba hatujawahi kumwona mwanamke mzuri kuliko huyu katika maisha yetu yote. Kwa kukubali mapenzi ya baba yake, Mtume s.a.w. alifunga ndoa naye kwa mahari ya dirhamu mia tano. Mtume s.a.w. alipokwenda kwake, yeye Asma akasema mimi nakuomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu (usiniguse). Mtume s.a.w. baada ya kusikia haya akasema: Umeomba ulinzi wa Mlinzi Adhimu na akatoka nje na kumwambia sahaba wake mmoja Abuu Usaidi kwamba msindikize mpaka nyumbani kwao. Tena historia imelihifadhi jambo hili pia kwamba wanafamilia wake walikuwa na furaha tele juu ya ndoa hii kwamba binti yao amepata bahati nzuri ya kuolewa na Mtume s.a.w. lakini yeye aliporudi nyumbani kwao, wanafamilia yake wakamchukia na kumkaripia. (*Maakhuz az atabakatul kubra leibne saad uk 318-319).*

Basi huyu ndiye yule mtukufu adhimu ambaye watu wanamsingizia masingizio ya bure kuhusiana na wanawake. Yeye alioa wake akifuata amri ya Mwenyezi Mungu. Hadhrat Masihi Mauud a.s. aliandika kwamba kama wasingepatikana wake wala wasingekuwepo watoto, basi khulka zake nzuri wakati wa majaribio aliyoyapata kutokana na watoto zisingepata kudhihirika wala khulka yake ya kuwatendea wake kwa wema isingebainika na kutufikia. Kwa neno zima kila tendo lake lilikuwa kwa ajili ya ridhaa ya Mwenyezi Mungu. (*Maakhuz az Chashmae Maarefat R.K jal 23 uk 300*)

Kuhusiana na Bi Aisha r.a. kuna masingizio kwamba alipendwa sana na vilevile maneno mabaya yanaelezwa kuhusu umri wake lakini Mtume s.a.w. anamwambia Bi Aisha r.a. "Katika baadhi ya mausiku nataka kumwabudu usiku kucha Mungu wangu ninayempenda zaidi kuliko vitu vyote". (*Aldurelmansuur jal. 7 uk 350*).

Hivyo basi, wale ambao akili zao zimejaa uchafu mtupu watatoa masingizio haya na kama walivyoendelea kutoa na huenda wataendelea kufanya harakati hizi siku za usoni kama nilivyokwisha eleza kabla. Mwenyezi Mungu ameisha kusudia kwamba Ataijaza jahanamu na watu wa namna hii.

Basi watu hawa na wasaidizi wao wanatakiwa kuiogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu kama Hadhrat Masihe Mauud a.s. alivyosema kwamba Mwenyezi Mungu Anaonesha ghera kubwa kwa ajili ya wapendwa wake. (*Maakhuz az taryaqul qulub R.K jal 15 uk. 378*)

Katika zama hizi Mwenyezi Mungu Ameielekeza dunia kwenye kujirekebisha kwa kumtuma Masihi na Mahdi Wake a.s. lakini kama wasipojizuia na mzaha na dhuluma basi makamato ya Mwenyezi Mungu ni makali sana. Siku hizi mabalaa yanashuka katika kila sehemu ya dunia na maangamizi yameenea kila upande, matufani yanatokea Marekani na yanazidi kuwa makubwa na mengi, hali mbaya ya kiuchumi inaendelea kuongezeka; kutokana na joto la dunia kuongezeka sana, kuna hatari kubwa ya maeneo fulani kuzama majini, maeneo haya yamekumbwa na hatari hizo; hivyo basi hao walioruka mipaka wanahitajika kumwelekea Mwenyezi Mungu. Mambo hayo yote yawe yenye kuelekeza kwa Mwenyezi Mungu sio kwamba waelekee kwenye upuuzi wa namna hiyo. Lakini kwa bahati mbaya mambo yaliyo kinyume na haya yanatendwa na zinafanywa juhudi za kuiruka mipaka wakati Imamu wa zama hizi amekwisha eleza na kuonya kwa uwazi sana kwamba watu wasipoifuata sauti yake, basi kila hatua yao itawasogeza karibu na maangamizo. Ujumbe wa Hadhrat Masihe Mauud a.s. ni ujumbe wenye kurudiwa mara kwa mara na unarudiwa mara nyingi sana basi leo tena ningependa kuuweka mbele yenu.

Alisema: "Ikumbukwe kwamba Mwenyezi Mungu Amenipasha habari ya matetemeko ya ardhi yatakayoendelea kutokea. Basi fahamuni kwa yakini kwamba sawa na bishara, kama vile matetemeko ya ardhi yalivyotokea Marekani, na katika Ulaya pia matetemeko ya ardhi yatatokea katika maeneo mbalimbali ya Asia na baadhi yao yatakuwa ni mfano wa Kiama na vitatokea vifo vingi kiasi hiki kwamba mito ya damu itatiririka. Kifo hiki kitawazunguka hata wanyama na ndege. Na ardhini yatafanyika maangamizo makali kiasi hiki kwamba tangu aumbwe binadamu, maangamizo ya namna hii yatakuwa hayajatokea wakati wowote na mahali pengi patateketea vibaya kana kwamba hapakuwa na watu wowote wakati wowote. Pamoja na haya yote, maafa mengine yatadhihirika mbinguni na ardhini kwa sura ya kutisha mpaka kila mwenye akili atayachukulia kama mambo yasiyo ya kawaida na katika vitabu vya falsafa na vya angani hamtakuwa na habari yoyote ya hayo. Ndipo watu watashtuka kwamba ni nini kitakachotokea na wengi wataokoka na wengi wataangamizwa. Zimekaribia zile siku bali naona kwamba zipo mlangoni ambapo dunia itashuhudia dhihirisho la kiama kimoja na sio matetemeko ya ardhi tu bali mabalaa mengine yenye kutisha yatadhihirika, baadhi kutokambinguni na mengine kutoka ardhini. Kwa sababu mwanadamu ameacha kumwabudu Mola wake na ameiangukia dunia kwa moyo wote, nguvu zote na mawazo yote. Kama ningekuwa sijafika, mabalaa haya yangechelewa kidogo lakini baada ya kufika kwangu, mipango ile ya siri ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iliyokuwa imefichika kwa muda mrefu sana, imedhihirika. Kama Asemavyo Mwenyezi Mungu "Nasi si Wenye kuadhibu mpaka tumtume mtume" (Bani Israel aya 16). Na wenye kufanya toba watapata amani na wale wanaoogopa kabla ya balaa kutokea watarehemiwa. Je mnadhani kwamba mtasalimika na matetemeko haya ya ardhi au mnaweza kujiokoa kwa mipango yenu? La hasha. Siku hiyo kazi za binadamu zitamalizika. Msifikiri kwamba matetemeko makali ya ardhi yalitokea huko Marekani na kwingineko lakini nchi yenu imesalimika nayo..... Ee Ulaya huko salama na ee Asia nawe huna amani na enyi wenye kuishi visiwani, mungu yeyote wa bandia hatawasaidieni. Mimi naiona miji ikiporomoka na nayakuta makazi yasiyo na watu. Yule Mungu Mmoja asiye na mfano alinyamaza kimya kwa muda mrefu sana, matendo yachukizayo yalitendwa mbele ya macho yake naye akakaa kimya lakini sasa ataonesha uso wake kwa matisho. Mwenye masikio naasikie kwamba wakati huo hauko mbali. Mimi nilijaribu kuwakusanya wote chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu lakini ilikuwa lazima yatokee yale yaliyokadiriwa.....". Anasema: "Zama za Nuhu zitakuja mbele ya macho yenu na mtashuhudia tukio la ardhi ya Luti kwa macho yenu wenyewe. Lakini Mungu Hatoi adhabu haraka. Kwa hiyo tubuni ili mrehemewe. Yule anayeachana na Mwenyezi Mungu ni mdudu sio mwanadamu na yule asiyemwogopa ni mfu sio hai" (*Haqiqatulwahyi jal. 22 uk 268-69*).

Mwenyezi Mungu Awape watu akili ili waweze kuepukana na kutenda matendo yachukizayo na ya kidhuluma na Mwenyezi Mungu Aendelee kutuwezesha pia kutekeleza wajibu wetu. Amin.

Filamu inayokashifu Islam yalaaniwa

Kutoka uk. 12

na amani ya nchi hizo, na fimbo ya Mwenyezi Mungu itakayocharaza ni jambo lingine. Kumbukeni kauli hii ya Imamu wa zama hizi kwamba kila ushindi hutoka mbinguni na mbingu imeshaamua hivi kwamba yule mtume mnayejaribu kumfedhehesha ndiye atakayeishinda dunia na kama alivyosema Hadhrat Masihul Maud a.s., atapata ushindi kwa kuishinda mioyo, kwani maneno matakatifu huathiri na hayahitaji kutumia ukiukwaji wa mipaka au kujibu upuuzi kwa upuuzi. Na mazungumzo haya mabaya waliyoyaanzisha watu hawa, Inshaalah yatamalizika haraka na halafu baada ya maisha haya Mwenyezi Mungu Atawashughulikia watu hao.

Katika aya nilizozisoma mwanzoni, humo pia Mwenyezi Mungu Amewaelekeza waaminio kwenye majukumu yao, kwamba kazi yenu ni kumsalia Mtume huyo na kumuombea amani. Heshima na utukufu wa nabii huyu adhimu hautaathirika hata kidogo kwa upuuzi, dhuluma na mzaha wa watu hawa. Huyu ni nabii aliye adhimu kiasi hiki kwamba Mwenyezi Mungu na Malaika Wake pia wanamtumia rehema. Kazi ya waaminio ni kudumu kumsalia Mtume huyu na maadui wakizidi katika upuuzi basi Waislamu wazidi kumsalia Mtume s.a.w. kuliko hapo awali.

Allahuma swalli ala Muhammadin wa alaa aali Muhammadin, kamaa swallaita ala Ibraahiima wa alaa aali Ibraahima, innaka Hamiidun Majiid. Allahumma baarik alaa Muhammadin, wa alaa aali Muhammadin, kamaa baarakta alaa Ibraahiima, wa alaa aali Ibraahiima, Innaka Hamiidun Majiid.

Ee Allah! Mrehemu Muhammad na wafuasi wa Muhammad, kama ulivyomrehemu Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim, hakika Wewe Ndiwe Uhimidiwae, Utukuzwae. Ee Allah Mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad, kama Ulivyombariki Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim, Hakika Wewe Ndiwe Uhimidiwae, Utukuzwae.

Hii ndio Sala ya Mtume (Durud) na huyu ndiye nabii ambaye amekadiriwa kupata ushindi duniani. Hivyo pale Mwislamu Mwahmadiyya anapodhihirisha kero, huzuni na hasira juu ya upuuzi huu, vilevile awaelekeze watu wa namna hii na wale wenye madaraka katika nchi yake kujiepusha na kujizuia na upuuzi wa aina hii, na kila Mwahmadiyya anapaswa kufanya hivyo. Kwa ajili ya kuitanabahisha dunia, Mwahmadiyya anajitahidi kudhihirisha ukweli ulivyo tofauti na njama hizi na kuonyesha nyanja mbalimbali za haiba na mfano mwema wa Mtukufu Mtume s.a.w. Mwahmadiyya anajaribu kudhihirisha mfano huu uliobarikiwa kupitia kila tendo lake na kwa jinsi hii kuubainishia ulimwengu uhalisia wa mfano huu. Kwa hakika wanaume, wanawake, wadogo, wakubwa na watoto wanapaswa kuzama katika kumsalia Mtume zaidi ya vile walivyofanya zamani, anga yote ijazwe na dua zao hizo. Kila mmoja ayafanye matendo yake yawe mfano halisi wa mafundisho ya Islam. Basi huu ndio upingaji mzuri tutakaoonesha.

Kuhusiana na mwisho wa wadhalimu hawa, Mwenyezi Mungu ameeleza katika aya nyingine kwamba wenye kumwudhi Mtume s.a.w. au wenye kuijeruhi mioyo ya waaminio kwa kumkashifu Mtume s.a.w., Mwenyezi Mungu atapambana nao Mwenyewe. Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya watu hawa katika dunia hii na kwa sababu ya laana hiyo,wataendelea kuzama zaidi katika uchafu na Mwenyezi Mungu amewaandalia watu hawa adhabu ifedheheshayo huko akhera. Hadhrat Masih ul Maud a.s. amebainisha jambo hili aliposema kwamba mwisho wa watu wa namna hiyo wenye lugha chafu hauwi mwema. Basi watu hao wataulaki mwisho wao mbaya hapa duniani kwa sura ya laana ya Mwenyezi Mungu na huko akhera kwa sura ya adhabu ifedheheshayo.

Waislamu wengine pia, sawa na mafundisho na amri ya Mwenyezi Mungu, wanatakiwa kuonesha upingaji huu kwamba wazijaze nchi zao, maeneo yao na mazingira yao kwa maombi ya kumsalia Mtume s.a.w. Huu ndio upingaji sahihi. Upingaji unaopelekea kufikia wazichome moto mali zao katika nchi zao wenyewe au wawaue wananchi wenzao au polisi walazimike kuwapiga risasi wananchi wenzao wanaofanya maandamano na kuwaua, haufai hata kidogo. Habari zitokanazo na magazeti na vyombo vingine vya habari, zinaonesha kwamba watu wengi wenye tabia njema wa Magharibi, pia wamekichukia sana kitendo hiki. Watu ambao si Waislamu lakini tabia yao ya asili inao wema ndani yake, hawajakipenda kitendo hiki huko Marekani wala hapa Uingereza.

Hata hivyo kwa upande mmoja uongozi unasema kuwa kitendo hiki si sahihi lakini upande mwingine kwa kutumia kivuli cha uhuru wa kusema, unakiunga mkono kitendo hiki. Mwenendo huu wa viwango viwili hauwezi kukubalika hata kidogo. Kanuni kuhusu uhuru wa kusema si sheria ya kimbingu. Mimi niliwaambia wanasiasa katika hotuba yangu huko Marekani hivi karibuni kwamba kanuni zinazoundwa na wanadamu zinaweza kuwa na kasoro na makosa ndani yake. Wakati wa kuunda kanuni, baadhi ya mambo yanaweza kumponyoka mwanadamu kwani mwanadamu hanayo elimu ya ghaibu, ila Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua ghaibu na kanuni Zake hazina kasoro ya aina yoyote ile. Hivyo basi, msidhani kwamba kanuni zenu ni kamilifu zisizoweza kubadilishwa. Ipo kanuni ya uhuru wa kusema lakini kanuni hii haipo katika katiba ya nchi yoyote wala katika mkataba wa Umoja wa Mataifa kwamba mtu yeyote hatakuwa na uhuru wa kuzishambulia hisia za kidini za mtu mwingine. Haikuandikwa popote kwamba hakutakuwa na uhuru wa kuwadhihaki watawa wa dini nyingine maana kutokana na hilo, hali ya amani ya dunia huharibika, volkano za chuki huchemshwa, umbali kati ya mataifa na dini mbalimbali huzidi kuwa mrefu. Kwa hiyo, kama kanuni ya uhuru wa kusema imeundwa na bila shaka yoyote undeni kanuni ya kumpatia mtu uhuru wa kusema lakini msiunde kanuni ya kuzichezea hisia za mtu mwingine. Umoja wa Mataifa pia unashindwa kwa sababu hii tu kwamba kwa kuunda kanuni zisizofaa wanaona kuwa wamefanya kazi kubwa sana. Tazameni kanuni ya Mwenyezi Mungu, Anasema kwamba msiyakaripie hata masanamu ya wengine maana kutokana na hilo, amani ya jamii huharibika. Ikiwa mtayakaripia masanamu nao pia bila kujua watatumia maneno yasiyofaa dhidi ya Mungu wenu Mwenye nguvu zote na kutokana na hilo, mtasononeka, chuki na hasira zitaongezeka, ugomvi na mapigano yatafanyika na ufisadi utatapakaa nchini. Basi haya ni mafundisho mazuri Anayoyafundisha Mungu wa Kiislamu, Mungu wa dunia hii, na Mungu wa ulimwengu huu. Mungu Yule anafundisha hayo Aliyemtuma mpendwa wake Hadhrat Muhammad s.a.w. kwa mafundisho yaliyokamilika kwa ajili ya kuiongoza dunia na kustawisha upendo na mahaba na Huyo Mungu kwa kumjaalia Mtume Muhammad s.a.w. lakabu ya rehema kwa walimwengu, Amemtuma akiwa rehema kwa viumbe wote.

Basi watu wa dunia walioelimika na wenye madaraka na wanasiasa wafikirie kwamba kwa kutowakemea kwao kwa ukali watu hawa wachache wapuuzi, wasije wakawa sehemu ya machafuko hayo. Watu wa kawaida wa dunia watafakari kwamba kwa kuzichezea hisia za kidini za watu wengine, na kwa kuwaunga mkono watu hawa wabaya waliozama katika uchafu, isije ikawa wanashiriki katika kuiteketeza amani ya dunia. Sisi Waislamu Waahmadiyya hatuachi nafasi yoyote ya kuitumikia dunia. Kulikuwa na mahitaji ya damu huko Marekani na mwaka jana sisi Waislamu Waahmadiyya tulitoa chupa elfu kumi na mbili za damu na mwaka huu tena wanakusanya maana siku hizi habari hizi zinatangazwa tena.

Mimi niliwaambia (watu wa Marekani) kwamba sisi Waislamu Waahmadiyya tunatoa damu zetu ili kuwapa watu uhai na nyinyi kwa harakati zenu hizi na kwa kuwaunga mkono wale waliofanya kitendo hiki kiovu mnatujeruhi mioyo yetu. Hivyo basi, hii ndiyo amali ya Mwislamu Mwahmadiyya na Mwislamu wa kweli. Na watu hawa wanaodhani kwamba wao ni wenye kusimamisha uadilifu, kitendo hiki kiovu kimefanywa na kundi moja wapo la kwao.

Waislamu wanalaumiwa kwamba wanachokifanya si sahihi. Ni kweli kwamba baadhi ya njia za upingaji si sahihi, kuvunja na kuteketeza mali, kuzichoma moto mali na majengo, kuwaua watu wasio na hatia, kutowalinda mabalozi, au kuwapiga au kuwaua, hayo yote sio sahihi. Lakini kuwadhihaki manabii watukufu wa Mwenyezi Mungu na kuzidi kutumia lugha chafu pia ni dhambi kubwa sana mno. Sasa baada ya kukiona kitendo hiki, siku chache zilizopita jarida la Kifaransa kwa mara nyingine tena limepata nguvu ya kuchapisha katuni za kipuuzi ambazo ni mbaya zaidi kuliko za awali. Watu hawa wa dunia wanafikiri kuwa dunia ndiyo kila kitu lakini hawaelewi kwamba dunia hii hii itakuja kuwaangamiza.

Hapa ningependa pia kusema hili kwamba katika sehemu kubwa ya dunia hii zipo tawala za Kiislamu. Maeneo mengi sana ya dunia yanatawaliwa na Waislamu, vilevile Mwenyezi Mungu Amezijaalia nchi nyingi za Kiislamu maliasili na nchi za Kiislamu pia ni sehemu ya Umoja wa Mataifa na ni wenye kuiamini na kuisoma Qurani tukufu ambayo ni mwongozo uliokamilika; basi kwa nini serikali za Kiislamu hazikufanya jitihada za kudhihirisha mafundisho haya mazuri kwa watu wa kila tabaka. Kwa nini hawafanyi hivyo? Sawa na mafundisho ya Kiislamu, kwa nini hawaliweki jambo hili mbele ya dunia kwamba kuzichezea hisia za kidini na kuwakashifu manabii wa Mwenyezi Mungu au kujaribu kufanya hivyo ni hatia na dhambi kubwa sana. Na ni muhimu sana kwa ajili ya amani ya dunia kwamba jambo hilo liwe katika mkataba wa amani wa Umoja wa Mataifa kuwa nchi yoyote ya Umoja wa Mataifa haitamruhusu mwananchi wake yeyote kuzichezea hisia za kidini za watu wengine. Kwa kutumia uhuru wa kusema, haitaruhusiwa kuiangamiza amani ya dunia. Ni jambo la kusikitisha kwamba haya yote yamekuwa yakifanywa kwa muda mrefu lakini nchi za Kiislamu hazijawahi kufanya jitihada madhubuti za pamoja kuifahamisha dunia juu ya heshima na utukufu wa manabii wote, pamoja na Mtume Muhammad s.a.w. na kulifanya jambo hili likubaliwe na mataifa yote. Ingawaje jambo hili pia halitatekelezwa kama vile ambavyo amri zingine za Umoja wa Mataifa kama vile mkataba wa amani usivyofuatwa, lakini angalau jambo hili litawekwa kwenye maandishi. Ipo OIC (Umoja wa nchi za Kiislamu) lakini haijabahatika kabisa kufanya juhudi imara ambayo kwayo heshima ya Waislamu iimarike duniani. Wanasiasa wa nchi za Kiislamu wanatumia kila njia kutimiza tamaa zao. Kama kuna kitu chochote ambacho hawakijali basi ni adhama ya dini. Kama viongozi wetu wangefanya juhudi imara, basi upingaji huu mkali wa watu wa kawaida pia usingedhihirika. Kwa mfano yale yanayofanywa siku hizi huko Pakistan na katika nchi zingine, huenda yasingefanywa kama watu wangejua kwamba viongozi wetu watalishughulikia suala hili na watajitahidi wawezavyo kulishughulikia vizuri, na kwa kuistawisha heshima na utukufu wa Mtume Muhammad s.a.w. na manabii wengine wote, watasimama imara kuieleza dunia kwa namna ambayo dunia itakubali na kuamini kuwa lolote wanalolisema ni la kweli na la haki.

Kisha katika nchi za magharibi na katika kila sehemu ya dunia, ipo idadi kubwa ya Waislamu wanaoishi, na kidini na kiidadi Waislamu ndio nguvu kubwa ya pili ya dunia. Kama Waislamu hawa wakifuata barabara mafundisho ya Mwenyezi Mungu, wanaweza kuwa nguvu kubwa kushinda zote kwa kila namna. Na kutokana na hilo, nguvu za maadui wa Kiislamu hazitathubutu kufanya harakati hizi zenye kuudhi moyo au kuwaza harakati hizo. Kwa vyovyote vile, mbali na nchi za Kiislamu, idadi kubwa ya Waislamu inapatikana katika kila nchi ya dunia. Katika Ulaya mamilioni ya Waturuki wanaishi, si katika Ulaya yote kwa ujumla tu bali katika kila nchi ya Ulaya wanaishi mamilioni ya Waturuki. Halikadhalika watu wa mataifa mengine ya Kiislamu wanaishi hapa Uingereza. Waislamu kutoka Asia wamekuja hapa, wanaishi U.K., Marekani, Kanada na wanaishi katika kila sehemu ya Ulaya. Kama hawa wote wakiamua kwamba watawapigia kura zao wanasiasa wanaoonesha maelewano ya dini, si kwamba wadhihirishe maelewano hayo ya dini kwa maneno matupu tu, bali wayaoneshe kwa matendo yao pia, na kwamba watawakemea wapuuzi wa aina hii au wale watumiao lugha chafu au wale watengenezao filamu (za aina hii); basi katika serikali hizi hizi za kidunia, litapatikana kundi moja lenye kuukemea na kuupinga upuuzi huu kwa uwazi.

Hivyo basi, kama Waislamu wakitambua umuhimu wao, mapinduzi yanaweza kutokea duniani na wanaweza kusababisha kuundwa kanuni zenye kuziheshimu hisia za kidini katika kila nchi. Lakini ni bahati mbaya kwamba hakuna mwelekeo wowote wa aina hii. Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya inayoelekeza, wanaipinga kwa nguvu zote na kuiimarisha mikono ya maadui. Mwenyezi Mungu awape akili viongozi wa Waislamu, wanasiasa na maulamaa ili waimarishe nguvu zao, watambue umuhimu wao na waelekee kwenye mafundisho yao.

Watu hawa wamsingiziao Mtume s.a.w. kwa masingizio ya kipuuzi, waliotengeneza filamu hii au waliohusikana nayo, kiwango chao cha maadili mema chaweza kujulikana kutokana na habari zao zilizochapishwa na vyombo vya habari. Inasemekana kwamba chanzo cha hayo yote ni Mkristo wa Kikibti anayeishi Marekani, aitwaye Nakoula Bassaley Nakoula, au kwa jina jingine anaitwa Sam Bacile. Kuhusiana naye imeandikwa kwamba anayo historia ya jinai yaani ni mhalifu. Mnamo mwaka 2010 alifungwa jela kwa sababu ya ulaghai. Mtu wa pili aliyeendesha filamu hii ni mwendeshaji wa filamu za kiponographia na waigizaji wengine wote ni waigizaji wa filamu za kiponographia. Basi hivi ndivyo viwango vyao vya kimaadili. Na ni vigumu kwa mtu wa kiponographia kuijua mipaka ya utu. Watu hawa wamezama katika uchafu wa namna gani. Wanataka kumsingizia yule mtukufu ambaye Mwenyezi Mungu Mwenyewe Ametoa ushahidi wa khulka zake tukufu na utakaso wake. Hivyo basi, kwa kufanya kitendo hiki kichafu, wao bila shaka wameichochea ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na wanaendelea kuichochea. Halikadhalika wafadhili wa filamu hii hawataweza kuepukana na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Miongoni mwa hawa yupo yule Padri wa Kikristo pia aliyekuwa anajaribu kuichoma moto Qurani huko Marekani katika nyakati tofauti kwa kujipatia umaarufu wa bure.

Ee Allah Uwaangamize kwa maangamizo makali na uwasage tikitiki.

Katika vyombo vya habari, baadhi ya watu wemejaribu kuipinga filamu hii na vilevile wameikemea njia ya upingaji ya Waislamu. Ni sawa kwamba upingaji usio sahihi unatakiwa kukemewa lakini hili pia liangaliwe kuwa ni nani aliyetangulia kukosea. Kama nilivyosema, ni bahati mbaya kwa Waislamu kwamba haya yote yanafanyika kwa sababu ya kukosekana kwa umoja na uongozi kati yao. Pamoja na madai yao ya kumpenda Mtume s.a.w., wamejitenga mbali na dini. Bila shaka wanayo madai lakini hawana elimu yoyote ya dini. Wanazidi kudhoofika kidunia pia. Nchi yoyote ya Kiislamu haijaonyesha upingaji wake kwa nguvu zake zote na kama upingaji umeoneshwa basi umeoneshwa kidogo kiasi hiki kwamba vyombo vya habari havijaupa umuhimu wowote. Na kama wamechapisha habari juu ya upingaji wa Waislamu, wamechapisha hivi tu kuwa: '**Bilioni**

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Muharram 1434 AH | December 2012 | Fatah 1391 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin 'Amr bin 'Aas r.a. ya kuwa Mtume s.a.w. alisema: Mwislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wanasalimika katika ulimi wake na mkono wake na Muhajir (Mhamaji) ndiye yule ayahamaye Aliyoyakataza Mwenyezi Mungu. (*Bukhari*)

Filamu inayokashifu Islam yalaaniwa

Filamu ya kashfa dhidi ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. iliyotengenezwa huko Marekani hivi karibuni imepelekea mtikisiko mkubwa duniani. Kiongozi wa Waaminio duniani, Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. katika hotuba yake ya Sala ya Ijumaa ya tarehe 21/9/2012 aliipatia dunia muongozo ufaao ili kulinda heshima ya dini zote na mahusiano mema baina ya dini na mataifa mbalimbali.

Baada ya Tashahhud na kusoma Suratul Faatiha, Khalifa mtukufu a.t.b.a. alisoma aya zifuatazo:

Tafsiri ya aya hizi ni: ***"Kwa Hakika Allah na malaika Wake wanamtumia rehema Mtume, enyi mlioamini, nyinyi pia mumsalie na kumtumia salamu. Kwa hakika wale watu wanaomuudhi Allah na mtume Wake, Allah Amewalaani duniani na pia akhera na Amewatayarishia adhabu yenye kufedhehesha."*** (Ahzab: 57-58).

Kisha akasema:

Siku hizi katika ulimwengu wa Kiislamu, ndani ya nchi za Kiislamu na hata kwa Waislamu waishio katika nchi mbali mbali duniani, kuna hali ya huzuni na hasira kali iliyosababishwa na kitendo kiovu, kichukizacho na cha kidhalimu cha maadui wa Islam. Kwa hakika Waislamu wanayo haki ya kudhihirisha huzuni na hasira hii. Mwislamu anakuwa yuko tayari kutoa mhanga uhai wake kwa ajili ya heshima na utukufu wa Mtume Muhammad s.a.w., kama ni mwenye kulitambua daraja la ubora wa Mtume s.a.w. au la.

Wale maadui wa Islam wametengeneza filamu ya kipuuzi na yenye kuchukiza dhidi ya Mtume s.a.w. na kwa jinsi walivyojaribu kumfedhehesha Mtume s.a.w. kwa njia ya kidhalimu, kuhuzunika na kukasirika kwa kila Mwislamu ni jambo la kawaida. Yule mhisani wa ubinadamu, rehema kwa walimwengu na mpendwa wa Allah, ambaye alikesha usiku kwa ajili ya kuwahuzunikia viumbe, na ambaye katika kuwaokoa wanadamu alidhihirisha uchungu mkubwa na kwa namna hii akajitosa kwenye huzuni kiasi kwamba Mungu wa Arshi Akamwambia: Je utaiangamiza nafsi yako kwa ajili ya watu hawa kwa kuwa hawamtambui Mola wao Aliyewaumba?



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a Khalifatul Masih V

Juu ya filamu hii iliyojaa fedheha dhidi ya mhisani huyu adhimu wa ubinadamu, bila shaka moyo wa kila Mwislamu ulikuwa usononeke na ndivyo ilivyotokea, na uchungu uliompata Mwislamu Mwahmadiyya ni mkubwa kuliko wote, kwani sisi ni miongoni mwa wale waliomuamini mpenzi wa kweli na mtumishi wa kweli wa Mtume s.a.w., Masihi Aliyeahidiwa a.s., aliyetufahamisha daraja adhimu la ubora la Mtume Muhammad s.a.w. Hivyo mioyo yetu imejeruhiwa vibaya na kitendo hiki na maini yetu yanakatika. Sisi twamsujudia Mwenyezi Mungu kwamba Awalipizie kisasi wadhalimu hawa. Awafanye kuwa ishara ile ya maonyo itakayobakia kuwa mfano daima dawamu.

Imam wa zama hizi ametufundisha namna ya kumpenda Mtume s.a.w. kwamba: "Inawezekana kufanya suluhu na majoka na wanyama wa porini, lakini hatuwezi kufanya suluhu na yule anayemfedhehesha bwana wetu aliye Khaatamul Anbiyaa, Hadhrat Muhammad s.a.w. na kuendelea kufanya hivyo. Waislamu ni watu ambao hujitoa mhanga kwa ajili ya heshima ya Nabii wao mtukufu s.a.w., nao wanaona ni bora wafe kuliko fedheha hii ya kufanya suluhu ya kweli na watu wa aina hii na kuwa rafiki zao, ambao kazi yao ya usiku na mchana ni kumtukana mtume wao mtukufu s.a.w. na kumtaja kwa fedheha na kwa maneno machafu kwenye majarida, matangazo na vitabu vyao."

Anaendelea kusema: "Kumbukeni kwamba watu wa aina hii huwa pia hawawatakii mema watu wao, kwa sababu wanawatia taabuni, nami nasema kwa ukweli kabisa kwamba, inawezekana tufanye suluhu na majoka ya porini na wanyama wakali wa jangwani, lakini hatuwezi katu kufanya suluhu na watu ambao hawajiepushi kuitolea maneno mabaya shani ya manabii watakatifu wa Mwenyezi Mungu. Wao wanadhani ushindi umo katika matusi na lugha chafu tu, lakini kila ushindi hutoka mbinguni."

Alisema: "Watu wenye lugha safi, hatimae huishinda mioyo kwa baraka za maneno yao matakatifu, lakini watu wenye tabia chafu hawana walifanyalo ila kusababisha mfarakano na vurugu nchini kwa njia ya fujo....."

Alisema "Uzoefu pia unashuhudia kwamba mwisho wa watu wenye lugha mbaya za aina hiyo huwa si mwema. Ghera ya Mwenyezi Mungu hatimae huonesha jambo fulani kwa ajili ya wapendwa wake hao." [*Chashma-e- Maarifat, Ruhani Khazain, jal. 23, uk. 385 – 387*].

Siku hizi pamoja na magazeti na matangazo, vyombo vingine vya habari pia vinatumiwa katika jambo hili la kipuuzi. Hivyo watu hawa ambao kutokana na ukaidi wao wanashindana na Mwenyezi Mungu, Inshaallah watakamatwa Naye. Wamejikita kwenye ukaidi na wanaendelea kudhihirisha kitendo chao cha kidhalimu kwa ujeuri.

Mnamo mwaka 2006, wakati watu wenye tabia mbaya wa huko Denmark walipochora picha za kumdhalilisha Mtume s.a.w., basi wakati huo niliwaelekeza Wanajumuiya kuonesha upingaji ulio sahihi, pia nilisema kuwa watu hawa wadhalimu waliendelea kupatikana hapo awali na hawataishia hapa. Maandamano haya na matendo mengine yanayofanywa sasa na Waislamu hayataleta mabadiliko yoyote, bali watu hawa wataendelea kufanya harakati za aina hii katika siku zijazo. Nasi twaona kwamba wamezidi katika kufanya dhuluma na upuuzi na tangu wakati ule desturi yao hii inaendelea tu kukua taratibu. Bila shaka kushindwa kwao mbele ya dini ya Kiislamu ndiko kunakowahamasisha kufanya mambo ya kipuuzi kwa jina la uhuru wa kusema. Kama vile alivyoeleza Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba kumbukeni kuwa watu hawa sio wenye kuwatakia mema hata watu wao. Jambo hili siku moja litawadhihirikia watu wa kaumu hizo. Itawadhihirikia kwamba upuuzi wowote waufanyao leo ni wenye kuiletea hasara kaumu yao. Watu hawa ni wenye kujipendelea na wadhalimu, mbali na kutimiza matamanio yao, hawajali jambo lingine lolote.

Wakati huu, kwa jina la uhuru wa kusema, wanasiasa na watu wengine, baadhi ya wakati kwa uwazi kabisa na mara nyingi kwa lugha za kificho, wanawaunga mkono watu hawa na wakati mwingine wanawaunga pia mkono Waislamu. Lakini kumbukeni ya kwamba dunia sasa imeshakuwa kama kijiji kimoja. Kama jambo baya halitasemwa kwa uwazi kuwa hilo ni jambo baya, basi mambo haya yataangamiza hata utulivu

Endelea uk. 11

Sheikh apata 'chamtemakuni' kwa kugombea mwili wa Marehemu

Na Mwl. Jafar Omar - Bungu
Jamaat, Rufiji Pwani

Bwana Ramadhani Likilima alifariki siku ya Jumanne tarehe 02/10/2012 katika hospitali ya Muhimbili - Dar es salaam ambako alikuwa amelazwa, na alizikwa siku iliyofuata siku ya Jumatano tarehe 03/10/2012 katika Kijiji cha Bungu Wilaya ya Rufiji mkoa wa Pwani.

Siku aliyofariki, dada yake alileta habari ya kifo chake kwa njia ya mawasiliano ya simu. Alinipigia simu na kunijulisha kwamba Bwana Ramadhani ameaga dunia ***'Innalillahi wa inna ilaihi raajiuun'*** (Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea). Ndipo nami nilipofikisha habari hizi kwa Rais wa Mkoa wa Pwani Bw. Yusuf Malinda. Naye alifanya mawasiliano na yule dada wa marehemu na kumfahamisha kuwa marehemu alikuwa ni ndugu yetu wa kiroho na kwa hivyo anastahili azikwe na ndugu zake Ahmadiyya. Yule dada wa marehemu alieleza kuwa yeye hakuwa na mamlaka yoyote bali wapo wenye mamlaka hayo ambao wangeweza kutoa kauli.
Baada ya ndugu hao kufanya kikao chao walileta kauli yao kwamba wanahitaji kumzika ndugu yao sawa na imani yao na taratibu zao, na kwamba hawataki kusikia habari ya kuwa ndugu yao (marehemu) alikuwa Ahmadiyya na hivyo azikwe na Waahmadiyya. Bali walisema Waahmadiyya wanaweza kuwepo kama waalikwa tu, lakini hawapaswi kuingilia taratibu za mazishi za marehemu huyo.

Hapo ujumbe wa Jamaat ukiongozwa na Rais wa Pwani Bw. Yusuf Malinda ulitoa jibu kwa ndugu hao kuwa si taratibu zetu kugombea maiti, bali kama wao wanang'ang'ania kuubeba mwili wa marehemu basi tunawatakia safari njema na tukaondoka.

Kesho yake iliwalazimu kuusafirisha mwili kuja kuzika kijijini Bungu. Siku hiyo mvua kubwa ilinyesha, hata walipofika na mwili wa marehemu iliwalazimu kuushusha mwili kutoka garini na kuuhifadhi ndani wakisubiri mvua imalizike ndipo waendelee na taratibu zao za mazishi.

Hata hivyo mara mvua ilipomalizika kukatokea mzozo baina ya wanandugu hao, kwani walikuwepo wengine waliotaka kuona haki ikitendeka. Hapo walihojiana wao kwa wao kuwa marehemu alikuwa Ahmadiyya sasa kwa nini ndugu zake wasipewe mwili wao kuuzika?

Hapo ilionekana walitaka kujirudi kosa lao ili watuombe msamaha na kutukabidhi mwili. Lakini kabla ya kufanya hivyo alisimama sheikh mmoja aitwaye Hamza Mohamedi Moko akasimama na kuwaamuru wafuasi wake wapatao 50 kwamba washike udhu ili wasali sala ya jeneza tayari kwa kumzika marehemu.

Wafuasi wakafanya utii huo na sala ya jeneza iliongozwa na Sheikh Hamza Mohamedi Moko mwenyewe. Baada ya sala hiyo kama ilivyo desturi ya Masuni kuongeza bidaa nyingi katika shughuli za mazishi. Hapo pia walianza kutia mapambio mbalimbali, Fatiha saba, Ikhlaswi tatu, n.k. Lakini Sheikh Hamza aliongeza vionjo zaidi! Yaa Ramadhani bin Ali Likilima 'ALLAHUMMAGHFIR LAHU WAR HAMHU WA ASKINAHU FII JANNA' wakati akiendelea na vimbwanga

Endelea uk. 9